

USHAWISHI WA MWINGINE



Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki.

Habari za jioni, marafiki, ni vizuri sana kuwa huku nje tena usiku wa leo Maskanini, kuzungumza tena kuhusu Bwana na Mwokozi wetu, ambaye sote tunapendana Naye nina hakika, ama hatungalikuwa tumeketi hapa katika jengo hili lenye joto, tukisongamana jinsi tulivyo usiku wa leo, kama hatukumpenda. Kwa sababu hilo ndilo kusudi letu la kuwa hapa, ni kumwonyesha ya kwamba tunampenda. Na matumaini yetu yana—yanatiwa moyo sana tunapowaza kuhusu wakati Wake unaokuja. Tunapona ishara zikionekana za kuja Kwake, tuna shauku ya ule wakati mkuu ambapo tutamwona.

² Tangu nilipokuwa hapa Jumapili ya juma lililopita, watu wengi zaidi wamelala mauti. Mmoja wao alikuwa Bi. Ford, Bi. Levi Ford. Alikuwa na umri wa miaka themanini, mwanamke mpendwa. Bwana yake alifariki hivi majuzi. Alikuwa mwanajeshi wa Vita vya Waamerika na Wahispaniola. Na katika hadithi ya maisha yangu nilitaja jina la mwanawe. Yeye ndiye ambaye ilikuwa anihifadhi ile suti, mwajua, baada ya kuchakaa, ile—ile suti ya—naamini ilikuwa suti ya skauti mwanamume. Naye... Nilipoenda kuchukua sehemu yake, kulikuwa tu na soksi moja iliyobaki.

³ Labda Lloyd yuko hapa usiku wa leo, kijana yule yule. Nami—niliendesha mazishi ya mamaye hivi majuzi. Naye akaniuliza, kasema, “Billy, ningependa ungalizungumzia jambo fulani linalohibitisha ya kwamba mama yangu atafufuka tena.” Naye Bwana akanipa ujumbe kwake ulio dhahiri, pasipo shaka... Wakati Biblia, maumbile yote, kila kitu alichoumba Mungu hunena habari zake, atafufuka tena. Nani—nani atakayepinga basi? Mungu amesema hivyo, anaithibitisha kwa maumbile Yake, anaithibitisha kwa Neno Lake, anaithibitisha kwa maisha Yake, kila kitu kinginecho, hana budi kufufuka, mnaona. Hamna njia, hamna kitu... Mbingu na nchi huenda zikashindwa, mbali hayo hayatashindwa. Hana budi kufufuka tena.

⁴ Kisha hivi majuzi, msimamizi ambaye aliambatana nami, Bw. Baxter (wengi wenu mnamkumbuka; yeye alihubiri kutoka mumu humu jukwaani hili), mkewe alikufa ghafla kwa ugonjwa wa moyo. Naye amevunjika moyo sana na kuhuzunika; nami natumaini—natumaini mtamkubuka Ndugu Baxter katika maombi yenu mnapoomba, maana ni mmoja wa ndugu zetu. Naye anaishi Vancouver, British Columbia. Naye hajakuwa pamoja nami kwa miaka kadhaa. Nasikia mke wake alikuwa na kitu kama ugonjwa wa neva ama cho chote kile, hatimaye

kwa ghafla akashikwa na ugonjwa wa moyo na akaaga dunia. Hatuwezi kamwe kujua yatakuja wakati gani. Kisha wakati yanapo—Yeye anapoitana, lazima tuwe tayari. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa usiku wa leo.

⁵ Nilikuwa kwenye chumba cha kusomea pale—afisini, hasa, nikizungumza na Bw. Moore. Aliisha nishawishi... Nilikuwa...?... Nilikuwa nikijaribu kuepa Kutoa Shukrani; nilitaka kuwa na mkutano hapa wa Siku ya Kutoa Shukrani, ndiposa niende hata Shreveport. Bila shaka, ninge—ingekuwa vigumu kwangu kufaulu. Na mwishowe akasema, “Vema, kama una—una mikutano mitatu sasa na baadaye utakuwa na zile Muhuri Saba, basi ungetupa siku moja kwa vyo vyote.” Kwa hivyo mwishowe, tungempa ile Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili. Na sasa, nalimuahidi Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili. Basi itakuwa... Pentekoste itakuwa na umri wa miaka hamsini katika Louisiana kwenye—Siku ya Kutoa Shukrani. Alishuka miaka hamsini iliyopita katika Louisiana.

⁶ Sasa, kesho asubuhi tutasisitiza ya kwamba kila mtu asiye na—na shule ya Jumapili unayohudhuria... Namwona Ndugu yetu mpendwa Don Ruddell hapa, nami najua ya kwamba ana shule ya Jumapili asubuhi. Na labda kuna wahudumu wengine hapa kutoka humu karibu walio na shule ya Jumapili. Naam, tunawatakeni mwende kwa shule zenu za Jumapili kama mnazo. Basi iwapo huna shule ya Jumapili, nawe ungetaka kuwa pamoja nasi, nataka kuzungumza asubuhi, na kuweka ubao wa kuandikia, na kufundisha juu ya *Kimo Halisi cha Mtu Mkamilifu*, na kuichora katika—kwenye huo ubao, na kuonyesha masharti ya Mungu na jinsi tunavyofikia kimo kikamilifu cha—cha mtu mkamilifu mbele za Mungu.

⁷ Ndiposa kesho usiku, Bwana akipenda, nataka kunena juu ya somo la *Kiongozi Wangu*. Kwa hivyo iwapo wengine wenu walio nje ya mji... Nasi tunataka kujaribu kuanza hizi ibada mapema kama... Sijazungumza na mchungaji bado, bali ningependa mngalianzisha shule ya Jumapili mapema sana asubuhi. Na kanisa kesho usiku, labda, ikiwezekana, ianze saa 12:30 jioni ama cho chote kile. Na hiyo itawapa hao watu nafasi ile kwamba iwapo wangetaka kubaki... Tunaweza kuondoka labda saa 2:30, ndiposa wengine wao...

⁸ Nilikutana na bibi fulani leo ambaye anasafiri saa tisa ama kumi, yapata... Yeye alisema, tukitoka saa 2 ama 2:30, yeye angefika nyumbani yapata saa 8:30 ama saa 9 usiku, bwana wake huenda kazini... Kwa hivyo hatutakuwa tukifanya cho chote isipokuwa kupitisha wakati tu humu, kwa—kwa hivyo hebu na tuje kanisani mapema. Nasi hatuna... Mwajua, si lazima tuwe na taratibu ya hili; Mungu hana utaratibu, mwajua, Biblia...?... Kwa hivyo, tunatumaini ya kwamba nyote mko hapa, na—wote wawezao.

⁹ Basi, iwapo mna ibada zenu, kumbukeni, hii ni maskani ya madhehebu yote ambamo watu . . . ? . . . huja. Na wengi wa umati wetu ni wa watu wanaotoka nje ya mji.

¹⁰ Basi kukiweko na mgeni hapa, nataka kukuonyesha jambo fulani. Nami nimekuja tu jukwaani na sioni—sioni watu kumi niwajuao. Watu wangapi hapa wametoka nje ya mji wa Jeffersonville, inueni mikono yenu. Mnaona, asilimia tisini na tisa. Mwaona, mwaona? mnaona? Ni marafiki tu. Wangapi walio hapa wametoka umbali wa maili mia moja, inuenimikono yenu. Kuna asilimia hamsini wa hao, waliotoka umbali wa zaidi ya maili mia moja. Wangapi walio hapa toka umbali wa zaidi ya maili mia mbili, inueni mikono yenu. Tazama hapa! Umbali wa maili mia tatu, inue mikono yenu. Tazama hapa! Umbali wa maili mia nne, inueni mikono yenu. Tazama hapa! Umbali wa maili mia tano, inueni mikono yenu. Angalieni hapa, zaidi ya theluthi moja ya kusanyiko hili umbali wa maili mia tano! Mnaona, ni marafiki tu wanaokusanyika kutoka kila mahali . . . ? . . . tutakuwa hapa. Kwa hivyo tunashukuru kwa ajili yenu, na tuko hapa kuwasaidieni. Tuko hapa kuwafanyia yote tuwezayo.

¹¹ Na sasa, nilikuwa nikisoma kule nyuma ba—barua mwanangu amenipa ya bibi aliyesema a—akija wakati huu itakuwa safari ya thelathini na tano ambayo amefanya akitumainia kuombewa. Amesafiri mara thelathini na tano maili mia kadha, mara thelathini na tano.

¹² Kisha kumbuka pia, kuna watu kama mia sita na kitu wanaongoja kwenye . . . ? . . . orodha ya wanaongoja toka kote ulimwenguni wakijaribu kupata mahojiano. Mnaona . . . ? . . . inatatiza sana. Tunapofikiria papa hapa, sio wengi sana. Tunesikia tu kwamba . . . Ona, ni ulimwenguni kote . . . ? . . . Na kwa hivyo sisi . . .

¹³ Nashangaa iwapo huyo bibi yuko humu jengoni usiku wa leo (safari ya thelathini na tano), aliyeandika barua ya kwamba angekuwa hapa kesho? Amekuwa hapa mara thelathini na tano bila kuombewa. Nakisia hayumo jengoni, labda hata hakuwahi kuja. Bali nilikuwa tu nikisoma barua yake kule nyuma.

Basi, nimejaribu kila mara ninapokuja humu . . . Ninapokuwa kule nyumbani, kuzungumza juu ya kitu fulani si niwe nazungumza tu, ama si jambo ambalo lingewafurahisha watu . . . Nimejaribu kuzungumza kuhusu jambo fulani ambalo lingalimpendeza Mungu na kuwasaidia watu (mwaona?), kwa msaada, kusudi sisi sote, haidhuru wewe ni wa kanisa gani, dhehebu gani, kusudi upate kusaidiwa kutembea pamoja na Mungu. Na hiyo ndiyo sababu yetu ya kuwa hapa: kutembea pamoja na Mungu.

¹⁴ Na tunapoona kwamba siku imechelewa kama ilivyo, na kukaribia kwa kule kuja kwa Bwana . . . Nilimwambia mke

wangu leo, “Kama sitaingia kwenye ufufuo mahali fulani, ni—nitaangamia; si—siwezi kuiyumilia kamwe. Mimi. . . Kitu fulani ndani yangu kinawasha.”

¹⁵ Lo! Tumetoka kwenye mfululizo wa mikutano ambayo maelfu ya watu walihudhuria. Na haidhuru kama ulikuwa na watu milioni mbili au tatu, iwapo hamna ufufuo, huo ndio tuliozoea kuiita kule Kentucky, mkutano wa mfululizo. Mwajua sote huenda kwenye kile tungeita mkutano wa mfululizo. Nasi tunataka ufufuo ambapo Roho wa Bwana anatenda kazi kati ya watu, na watu wanaokolewa, na mambo makuu yanatendwa kutimiza jambo fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

¹⁶ Na sasa, katika ibada za maombi, kwa kawaida, sisi. . . Unaweza kuona kwa nini hatungeweza kufanya mstari wa maombi hapa. Unaona, tumesongamana sana, haungeweza kufanya hivyo. Waona? Lakini kwa kawaida katika mistari ya maombi ni watu ambao—wanakuja na kuona Bwa—Bwana ni wa kweli. Nasi twaona ya kwamba Bwana Yesu hajakabadilika hata kidogo. Vile alivyokuwa, ndivyo alivyo leo, na atakuwa hivyo daima. Na Biblia ilisema katika Waebrania 13:8, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na katika makusanyiko ya watu waliokutanika kumsikiza katika siku hizo, labda hawangaliingia katika mstari wa maombi; bali wangukuwa na imani ya kuamini. Naye Bwana wetu angegeuka, wakati imani yao ilipomgusa, naye angegeuka, na kuwaambia watu ya kwamba walikuwa wametenda mambo fulani mabaya, na kwamba waende wakaonywe, ama waende wakatende jambo fulani, warekebishe jambo fulani ama cho chote kile.

¹⁷ Tunajua habari za yule mwanamke kisimani, ya yule mwanamke aliyetokwa na damu, na, lo, wengi sana, Bartimayo kipofu, ambao imani yao ilimgusa. Na usiku wa leo Yeye yungali Kuhani Mkuu wa maungano yetu na ni mkuu tu kama alivyowahi kuwa. Naam, inatupasa kujitolea wenyewe kuwa watumishi Wake. Yeye ndiye Mzabibu, cha—chanzo cha Uzima. Sisi ni matawi tunaopokea huo Uzima. Na matawi ndiyo huzaa matunda, si mzabibu. Na sasa, Kristo hutenda kazi kupitia kwa Kanisa Lake. Ndiposa, kama tungaliweza kujitolea wenyewe hivi kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuchukua mamlaka yote juu yetu katika imani yetu kwa Kristo, Yeye atatenda jambo lile lile, maana ni Kristo.

¹⁸ Na ikiwa uko hapa mgeni pamoja nasi. . . Sasa, kwa kawaida watu hapa. . . ? . . . maskanini. . . Mchungaji wetu hapa huwaombea wagonjwa karibu kila usiku, nawe upate kuombewa na Mchungaji wetu mwenye neema na tunayempenda, Ndugu Neville, mtu ambaye Mungu humsikia na kujibu maombi yake, Ndugu Orman Neville. Na—na Ndugu Don Ruddell, na ndugu hao wengine wanaowaombea wagonjwa. . . Na Ndugu Jackson, nakisia yuko hapa mahali fulani kutoka kanisa shirika kule Howard Park.

¹⁹ Na wakati huu ambapo—ambapo tumesongamana hivi, kama tu utamwamini Mungu . . . ? . . . cho chote unachohitaji . . . Nawe ni mgeni nami sikujui, hebu muombe Mungu tu uone kama Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele. Uone kama Yeye hawezi kurudisha maneno . . . ? . . . Yeye anakujuu; anajua shida yako ni nini; jambo tu likupasalo kufanya ni kumwamini tu. Ndiposa, Yeye atakutumia kama chombo kimoja nami kingine. Yesu alisema, Yohana Mt. 14:7, “Yeye aniaminiye MIMI, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Naam, hicho ni chombo kilichojitolea.

²⁰ Kesho tutafundisha jinsi unavyofanyika chombo hicho, kusudi Mungu, Roho Mtakatifu anaweza kutenda kazi kupitia kwako. Na kwa hivyo . . . Waona, Yeye hapo kale . . . ? . . . Mungu alikuwa katika nguzo ya moto, kisha akawa—akakaa katika Mwanawe, Kristo Yesu; sasa katika Kanisa Lake. Wakati mmoja Yeye alitwa Baba, kisha Mwana, sasa Roho Mtakatifu. Ni Mungu akijitokeza Mwenyewe kwa ulimwengu. Njia ya pekee Yeye angaliingia katika Kanisa ilikuwa kwanza kulifia Kanisa apate kulitakasa, ili apate kujitokeza Mwenyewe kupitia kwa Kanisa Lake. Ndipo akasema katika Yohana Mt. 15, “Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi,” (mwaona?), nayo matawi huzaa tu matunda. Bwana awabariki.

²¹ Na sasa, kabla sisi . . . Kwa ajili ya somo hili usiku wa leo . . . Nami sitaki kuwaweka kwa muda mrefu, maana naona watu wamesimama, na mmoja akichukua mahali pake, kisha mwingine anaketi chini, na kadhalika. Tunajaribu sana kupata ru—ruhusa ya kuketisha yapata watu mia tatu au mia nne zaidi, lakini yaonekana kwamba mji unatuzuia kufanya hivyo, kwa maana hatuna nafasi ya kutosha kupaki motokaa. Tulipata ruhusa kutoka Indianapolis, halafu mji . . . Hatuna budi kuwa na nafasi ya kupaki. Lo, tunapowaingiza watu wanne humu ndani, hatuna budi kuwa na nafasi ya kutosha kuweka motokaa hapa nje. Na mahali hapa pa kupaki bila shaka ni mali ya mji huu, kwa hivyo, mwaona, wao . . . Sisi tu—kanisa letu hapa ni kama tu futi moja kutoka mpaka wa mji. Na—bila shaka, barabara kuu, sababu ya kunjengwa pale . . . Bila shaka, baadhi yenu watu, vijana hapa, hamngalielewa hili, bali hapa palikuwa kidimbwi. Nami nakumbuka nilipokuwa kijana, tungeenda kule, nasi ilitubidi kuzunguka kule uwanjani kukifikia hicho kidimbwi. Wao walijenga barabara—kuzunguka barabara—kuzunguka hicho kidimbwi.

²² Na, nilinunua sehemu hii hapa. Nikiomba papa hapa ambapo hii imesimama, Bwana aliniambia nipanunue yapata miaka thelathini iliyopita, au miaka thelathini na miwili iliyopita nafikiri hivyo. Papa hapa katika ziwa la matope kubwa mno na majani marefu juu ya kichwa changu . . . nami nikakinunua kipande hicho cha ardhi kwa dolla mia moja na sitini, hii kona—konani papa hapa, na kujenga kanisa hili.

²³ Basi, Bwana awabariki. Nataka (kama lingelitwa fungu la maneno, kwa ajili ya baadhi ya . . .), kusoma maneno yenyewe kutoka kwa muhtasari; ningetaka kuwazungumzia wasikizi usiku wa leo juu ya somo la *Ushawishi wa Mwingine*. Na kabla hatujanena ama kusoma Neno, na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Mwandishi wa Neno.

²⁴ Basi, huku vichwa vyetu vimeinamishwa na mioyo yetu . . .? . . . pia katika unyenyekevu Wake mtakatifu, nashangaa iwapo kuna wengine . . .? . . . usiku wa leo ambao wana haja ambayo—inayowawasha moyoni mwao, kwamba wainue tu . . .? . . . mikono yao mbele za Mungu na kusema katika maombi yenu, “Bwana Yesu, nina haja. Nena nami usiku wa leo. Niponye. Nipe mahitaji yangu ya kifedha,” ama cho chote kile. Yeye hutupatia kila tunachohitaji. Mungu awabariki. Yapata asilimia tisini ya kusanyiko.

²⁵ Baba yetu uliye Mbinguni, tunakukaribia Wewe. Sasa tunapoondoka kwenye haya maskani ya udongo tunamoishi, chombo hiki kidogo kinachoelea katika bahari ya maisha, kwa imani tunapaa juu mbele ya sayari ya Mars, Jupiter, Venus, mwezi, nyota, makundi ya nyote, na kuwasili sasa kwa imani kwenye kiti cha enzi cha Baba. Tunamwona ameketi pale, mikono Yake iliyochoywa na miguu Yake; na hiyo damu sasa ifanye upatanisho tunapoweka sadaka zetu juu ya madhabahu ya dhahabu karibu na kiti Chake cha enzi.

²⁶ Tunakushukuru kwanza kwa ajili ya Yesu, aliyefanya mambo haya yote yawezekane kwetu kwa imani yetu tutakayoomba. Wewe uliiona hiyo mikono, ulijua kile kilichokuwa kikipigapiga moyoni mwa hawa watu. Nami naweka imani yangu Bwana juu ya sadaka katika yale madhabahu makuu ya Mungu ya dhahabu ambamo uvumba unachomwa kila siku. Naomba ya kwamba utayasikia na kuyajibu maombi yao, Baba. Wape haja za mioyo yao.

²⁷ Na sasa, kama vile tumekusanyika, Bwana, usiku wa leo hii mikutano mitatu, tuko hapa katika jengo hili lenye joto usiku wa leo si kwa kusudi lingine bali kutembea pamoja na Wewe. Tukijua la kufanya . . .? . . . Bwana, la kufanya . . . Kama alivyosema nabii, “Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya. Watapanda juu kwa mbawa kama tai. Watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.” Bwana, tufundishe jinsi ya kungoja baada ya sisi kuomba na . . .? . . . kuwa na imani kujua ya kwamba Wewe ulisikia, na katika wakati Wako ufaao utatutumia majibu kupitia vipandio vya dhahabu kutoka kwenye ukumbi wa Mbinguni kuingia moyoni mwetu. Nasi tutapata tuliyoomba, kwa maana tunaamini.

²⁸ Yatakase masikio yetu kusikia na mioyo yetu kupokea; hebu kwamba ibada itakapokwisha, tuweze kusema kama wale

waliotoka Emau, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani.” Kwa maana tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

²⁹ Ningetaka kusoma usiku wa leo sehemu ya Maandiko inayopatikana katika Kitabu cha Isaya. Kesho, hakikisha kwamba iwapo una karatasi nawatakeni m...Nitakuwa na mchoro hapa ama ubao kuchora somo langu. Na nawatakeni muipate mkiweza, kwa maana mwaweza kuisoma mfikapo nyumbani.

³⁰ Isaya sura ya 6, nataka kusoma vifungu vichache kutoka katika sura hii kupata somo kwa—kwa ajili ya usiku wa leo.

*Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona
Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana
na kuinuliwa sana, na pindo za vazi Lake zikalijaza
hekalu.*

*Juu Yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa
na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa
mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.*

*Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema,
Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa
majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.*

*Na misingi ya visingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti
yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.*

*Ndipo niliposema, Ole wangu! kwa maana nimepotea;
kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na
nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na
macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.*

*Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia;
naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo
alikuwa amelitoa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;*

*Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia,
Tazama, hilo limekugusa midomo yako, na uovu wako
umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.*

*Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume
nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?
Ndipo niliposema, Mimi hapa; nitume mimi.*

³¹ Hii ni—ni kazi kubwa tunapowazia juu ya—nini itakachomaanisha tuchunguzapo hili ono la Isaya. Ni...Daima nimempenda Isaya. Yeye alikuwa mmoja wa manabii walio wakuu. Isaya aliandika Biblia nzima. Kuna Vitabu sitini na sita katika Biblia, na Isaya aliandika sura sitini na sita. Yeye anaanza na mwanzo wa uumbaji; katikati ya hicho Kitabu analeta Agano Jipya na Yohana Mbatizaji; kwenye sura ya 56 na ya 60 yeye anamalizia katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu: Mwanzo kupitia kwa Agano Jipya hata Ufunuo. Huyu Isaya

alikuwa mtu mkuu. Mwishowe alikufa kama mfia imani chini ya adhabu ya kifo.

³² Kila mtu wa Biblia aliyejazwa Roho alikufa ama aliteswa chini ya serikali kuu ya nchi. Kila mmoja wao unayeweza kumwazia: Musa, wale wana wa Waebrania, Danieli, na Isaya. Isaya alikatwa vipande—vipande kwa msumeno. Na kuendelea, Yohana Mbatizaji, kila mmoja wa mitume, Yesu Mwenyewe, wote walikufa chini ya adhabu ya mauti ama kuadhibiwa na serikali kuu ya nchi. Na kulingana na vile mambo yanavyolundikana, shuhuda zingine zitaongezwa kwa zao hivi karibuni. Mwaona? Na iwapo kulikuweco na wakati tulipopaswa kuungana, ni sasa.

³³ Nakisia mmesikia kuhusu mkutano unaoendelea kute Rumi, nasi tuna—nao wana wakati mkuu sana huko. Nao wataanzisha ufufuo. Na utakuwa ufufuo wa dunia nzima, bila shaka.

³⁴ Turudie somo hili (tutapata hayo katika Mihuri Saba)—turudie somo hili la kushawishiwa.

Mfalme Uzia alikuwa mvulana mchungaji. Yeye alilelewa. . . Naye alitaka kuwa nje. Naye alitawala katika siku za unabii wa Isaya. Isaya alijifunza kutoka—kutoka mmoja wa wale manabiii wengine walio wakuu. Nami naamini ilikuwa Zekaria, ambaye Isaya alipata ufahamu kwake, ambaye alikuwa nabii wakati Isaya alipojitokeza. Naye Isaya aliitwa, naye alikuwa na—nabii. Manabii hawafanywi na wanadamu; manabii huzaliwa manabii.

³⁵ Naam, kuna karama ya unabii inayokuja kanisani, ambapo watu hutoa unabii. Washiriki wengi wa Mwili wa Kristo wangepanya hayo, ambao wamo chini ya upako. Bali nabii anawekwa Kanisani na Mungu, amechaguliwa tangu asili karama hiyo ya—ya nabii—ama karama kuwa nabii, si mtabiri.

³⁶ Naam, basi, tunaona ya kwamba huyu kijana alikuwa ametawazwa. Iwapo unataka kuandika baadhi ya hayo Maandiko, ni 2 Mambo ya Nyakati sura ya 26. Unaweza kusoma ambapo inasimulia ya kwamba Mfalme Uzia baada ya kifo cha babaye A-m-a-z-i-a, Amazia—baada ya kufa, akiwa mtu mwenye haki naye alikuwa amemwacha Bwana, kisha akauawa na watu wake mwenyewe—Uzikia alichukua—ama Uzia, namaanisha, akachukua mahali pake kama mfalme. Naye aliketi kwenye kiti cha enzi na kutiwa mafuta mwenye umri wa miaka kumi na sita, mvulana tu, bali ndiye alikuwa awe mfalme, ingawa alikuwa mvulana tu. Naye akafanya yaliyo mema. Biblia inatuambia ya kwamba yeye alikuwa na baba mcha Mungu na mama mcha Mungu, naye hangalikuwa kitu kingine cho chote akiwa na ushawishi kama huo ila kuwa mvulana mcha Mungu, kwa sababu hicho ndicho kiliwekwa mbele zake wakati wote.

³⁷ Mwajua ninayofikiria? Kila mtu ana maoni yake. Bali mmoja wa marais wakuu sana, nionavyo mimi, rais mkuu sana tuliyeptata kuwa naye ni Abraham Lincoln. Sasa, si eti kwa sababu alikuwa wa chama cha Republican, bali

kwa sababu alikuwa kile alichokuwa, mtu mcha Mungu. Naye aliinuliwa, na yeye—amtumikie Mungu. Naye alisema, “Kama kuna kitu ninachotaka kushukuru kwa ajili yake,” akasema, “kilichoyashawishi maisha yangu, ni mama mcha Mungu aliyenifundisha kuomba na kumjua Yesu kama Mwokozi wangu.”

³⁸ Lo! Ilivyo jamaa yako ndivyo ulivyo. Unamlea mwanao katika mazingara fulani; ana nafasi nzuri ya kuwa mwema asili mia tisini na nane kuliko alivyo nayo kama ukimlea vibaya. “Mlee mtoto katika njia impasayo, naye atakapokomaa hataiacha.” Walee iwapasavyo, wafundishe watoto wako kutenda yafaayo: kuwa waaminifu, wawe wanyofu na wema hata wanapokuwa shuleni.

³⁹ Naam, wakati mwingi watoto huzoea kunakiliana wao kwa wao na kujaribu kujisukumiza shuleni. Lakini mwajua, nafikiri kama utaipata tu mwenyewe, basi hicho ni kitu ambacho uta—utafurahia karatasi yako yenye maksi nzuri.

⁴⁰ Wajua, kama unaenda kufanya mtihani siku inayofuata, badala ya kutangatanga usiku kucha, ukaamka asubuhi ifuatayo, na kuwazia, “Vema, nitaketi karibu na *Fulani na fulani*; wao ni werevu; kisha wata—nitanakili kutoka kwao,” kama ungetaka tu kabla Baba hajaombea kiamsha kinywa mezani, iwapo ungalisema tu, “Baba, nikumbuke leo, nitafanya mtihani wa kemia,” ama cho chote kile. Kisha nawe, Baba unapoomba, sema, “Mungu, mbariki Yohana, Mariamu katika mtihani wao leo.” Nakwambia, itabadilisha mambo.

⁴¹ Kumbuka, tunaweza kupata tunachohitaji ikiwa tutaomba kwa imani tukiamini. Yesu alisema, “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Hamna kitu kwa kuwa hamwombi, nanyi hamwombi kwa sababu hamwamini.” Akasema, “Ombeni sana ili furaha yenu itimizwe.” Nappenda hilo.

⁴² Mafundisho yetu yawe kweli: Sema kweli; fanya yaliyo kweli; wazia yaliyo mema; kila mara wazia yaliyo mema. Nami nina msemo mdogo:

Tenda yaliyo mema, huo ni wajibu wako kwa Mungu.
Wazia yaliyo mema, huo ni wajibu wako kwako mwenyewe; nawe hunabudi kuwa mwema.

⁴³ Hauwezi kuwa ukienda mashariki na magharibi wakati mmoja, wala hauwezi kuwa ukifanya mema na mabaya wakati mmoja. Haidhuru unavyofikiria unaenda upande ule mwingine, iwapo hauendi moja kwa moja magharibi. . . Huendi mashariki iwapo unaenda magharibi.

⁴⁴ Kwa hivyo huyu mfalme kijana alishawishiwa na babaye alipokuwa kijana mwanamume na kuwafundisha Israeli maagizo ya Mungu. . . Mara akabadilika katika siku zake za mwisho na kufundisha dhidi ya Mungu. Na watu wake. . . Yeye aliuawa na watu wake. Ilionekana kama kwamba hilo

linge kuwa onyo kali sana kwa Uzia juu ya hili. Bali twaona ya kwamba Uzia alipotwaa kile kiti cha enzi, alianzia vyema kama alivyofanya babaye, kurudisha mambo ya Mungu, kuwarudisha Israeli kwenye ibada ya Mungu. Akajiimarisha mwenyewe.

⁴⁵ Nami nataka daima kushukuru kwa ajili yake katika siku za ujana wake, kwa maana yeye hakuwa na hila za kisiasa. Ingawa huenda siasa zilimpinga, hata hivyo, yeye alidumu kabisa upande wa Mungu. Nayo ikamfurahisha sana maskini huyu nabii kijana, hata akawa shujaa wake. Yeye alikuwa kielelezo kwa nabii Isaya.

⁴⁶ Naye Isaya akaenda kwenye ile ngome kukaa pamoja naye, katika jumba la kifalme. Yeye alimwalika; alimpenda Isaya. Isaya alikuwa kijana pia, na—naye. . . Walikuwa marafiki sana. Na jinsi huyo mfalme. . . Alipokwenda kule, nao—baadhi ya wanasiasa wangukuja na kusema, “Inatupasa tufanye *hivi na vile*,” Mfalme Uzia kwanza alimtafuta Mungu. “Bwana, je, ni mapenzi yako kwamba tufanye *hivi na vile*?” Mungu atupe rais kama huyo, si huyo tu, bali atupe wahubiri. “Basi utafuteni Ufalme wa Mungu, na haki Yake; na mambo yote mengine yatazidishwa.”

⁴⁷ Hapana budi huu ulikuwa ushawishi mkubwa, kwa maana Isaya alimpenda, kwa maana aliona ya Kwamba yeye ni mtu mkuu, naye—naye alidumu dhabiti na imara kwa Mungu. Wajua, kila mara katika siku tunazoishi, katika mambo tutendayo, kumbukeni umma hawamtazami tu mchungaji jinsi anavyoonekana—anavyoishi, yeye—wao pia huwaangalia washirika.

⁴⁸ Lo, ni vibaya sana tunapowazia habari za kanisa. Mara kwa mara kama mchungaji ni wa dhehebu *fulani* ama kabila, na dhehebu hili limtume kwa kanisa *fulani*, na wakati mwingine mikono ya huyo mchungaji imefungwa na dhehebu hilo. Naye maskini mtu huyo anataka kumtumikia Bwana, naye anafikiri—ameisha fundishwa ya kwamba hivyo tu ndivyo anavyoweza kufanya, ni kulitumikia dhehebu lake. Naye kama angaliinuka na kuhubiri Neno lisemavyo, kanisa lingelimwondolea mbali; kisha yeye anaogopa hatapata nafasi ya kuhubiri Injili.

⁴⁹ Bali lo, tunachohitaji mimbarani leo ni watu kama Uzia alivyokuwa. Haidhuru siasa za kanisa lake ama siasa za cho chote kile, yeye alitenda mpenzi ya Mungu daima. Yeye alingoja hata akapata BWANA ASEMA HIVI, kisha akatenda.

Maskini. . . maskini nabii huyo (kijana wa karibu umri wake) wakiwa hekaluni pamoja, wangeshuka kwenda kule kuomba, bila shaka, na kutaka kujua mapenzi ya Bwana, halafu wakayalinganisha na sheria za Biblia. Bali ikiwa ilikuwa sawa, Uzia aliidhinisha; kama haikuwa kweli, yeye alihukumu siasa zake. Mungu atupe wengi walio hivyo! Na hilo lilifurahisha Isaya kwa sababu Yeye alikuwa nabii.

⁵⁰ Naye Uzia akawa shu—shujaa kwa Isaya. Unaona yeye alikuwa... Kwa sababu ya m—msimamo wake kwa Mungu, akawa shujaa mbele ya macho ya wenye haki. Na huenda hakukuwa na walio haki wengi sana. Waona? Bali jambo tunalotaka kuyafanya, ni kufanya maisha yetu yampendeze Mungu. Mtu fulani anakuangalia.

⁵¹ Nilikuwa nikimuonya mtu fulani hivi majuzi. Mahali fulani hapo karibu walikuwa na... Kanisa kubwa la kidhehebu lilikuwa na karamu ya rumba humu, nao walikuwa wakiiicheza hadi saa 7 usiku. Nao walikuwa wanamuudhi mtu fulani anayehudhuria maskani, na kusema eti hao ni watakatifu wanaofingirika wanaokuja humu, kwa maana hatuna dhehebu. Jamani, hilo lilinipa nafasi. Mwaweza kuwazia tu yaliyotendeka. Lakini jambo ni kwamba sasa watu hao... bila shaka huyo msichana aliyefanya hayo matamshi, laiti angalijua yaliyo Kweli...

⁵² Nilikuwa milimani majuma matatu yaliyopita. Na kule nyuma kabisa nilipokuwa nikija nyumbani, tukarudi (mimi na jamaa yangu) kupumzika kidogo, tunakokwenda tena, Bwana akipenda, juma lijalo. Halafu, kule nyuma wakati mmoja, nikaona ono. Na ilikuwa mwa—mwanamke, mwanamke mrembo sana, ilionekana kama kijana mwanamke anakimbia; alikuwa ameweka mkono wake hapa, naye alikuwa akiangamia kwa ugonjwa wa moyo, mwanamke mrembo. Naye akaanguka akafariki. Naye Malaika wa Bwana akasema, “Sasa, utakaposikia haya, kumbuka, watasema ya kwamba yeye alijiva, bali alikufa kwa ugonjwa wa moyo. Na ni karibu saa 10, kwa hivyo sema tu saa 10,” kisha akaniacha.

⁵³ Nami sikuwaamsha jamaa kwenye kile kibanda kidogo cha ng’ombe (ama mahali wachungaji wa ng’ombe huishi, ambapo tungeenda kule na kuwakusanya ng’ombe), ni—niliwaacha walale hata asubuhi. Ndiposa, siku iliyofuata nikataja hilo, nami nikasema, “Kijana mwanamke fulani, mwenye uso mzuri sana, atakufa kwa ugonjwa wa moyo.” Basi tulipokuwa barabarani siku mbili baadaye, ndiyo hiyo ikitangazwa radioni ya kwamba Binti (siwezi kulikumbuka jina lake) Monroe, Bi. Monroe. Nafikiri hilo ndilo lililokuwa jina lake la michezoni, ama cho chote kile; jina lake lilikuwa lingine. Naye alikuwa amekufa, nao wakasema ya kwamba alijiva.

⁵⁴ Naam, haidhuru nitasema mara ngapi; wao wataendelea kusema ya kwamba yeye alijiua. Bali mtoto huyo hakufanya hivyo; alikufa kwa ugonjwa wa moyo! Na kama ukitazama, alikuwa amenyosha mkono wake, akijaribu kushika simu—ameshika simu mkononi mwake. Alishikwa na ugonjwa wa moyo. Walisema dawa za usingizi zilikuwa pale; alikuwa akizinywa kwa mwezi mmoja (Mwaona?) au zaidi, kutoka kwa chupa. Alikufa kwa ugonjwa wa moyo, naye alikufa saa 10 kasoro sekunde nne tano, hasa.

55 Nami nikasoma hadithi ya maisha yake gazetini jinsi ambavyo. . . Alikuwa mwana haramu; na jinsi alisafisha vyombo vingi sana; mamaye akiwa katika hospitali ya wenda wazimu; naye alikuwa na hamu (bali alikuwa msichana mwenye umbo kamilifu sana, nakisia, ulimwenguni)—bali alionea shauku kitu ambacho pesa hazingeweza kununua. Nikawaza, “Lo, laiti ningalimfikia! Najua alichohitaji!” Ndivyo hivyo.

56 Huenda ikawa washiriki wa makanisa mazuri sana—yenye sifa za Holywood, ambamo mna mapambo yote na kumetameta. . . Bali wao waliwaona watu hao. . . Yeye angeona hawakuwa wakiishi maisha tofauti na yale aliyoishi. Inachukua ushawishi! Inachukua nguvu ya kufufuka Kwake Kristo kati ya watu, wapate kuona ya kwamba Kristo si sanamu inayoning’inia jengoni, bali Yeye ni Kiumbe kilicho hai katika umbo la Roho Mtakatifu, akiishi katika wanaume na wanawake, akileta amani, uradhi, na furaha. Jamani, laiti tungalimwendea maskini bibi huyu kabla hajaondoka ulimwenguni.

57 Sasa, ushawishi. Tunaona ya kwamba—ya kwamba maisha ya Uzia yalimshawishi nabii huyu hata kufikia mahali ambapo Uzikia—Uzia, namaanisha, alijenga kuta na kujiimarisha mwenyewe, na kuteka nchi pamoja na mali yao kutoka kwa Wafilisti, na kadhalika, hata sifa zake zikaenea hata Misri. Nami nawaambieni, katika mambo ya nyakati zote za wafalme, hamna hata mmoja nje ya Suleimani, aliyekuwa na sifa kama Uzia. kwani? Kwa sababu alionyesha mfano. Alidumu pamoja na Mungu, haidhuru watu wake walisemaje, yale ye yote aliyowazia, yale wanasiasa wake waliyojaribu kumshawishia. Yeye alidumu akijielekza kwa Mungu, na—Mungu akambariki. Ulikuwa msaada mkubwa sana kwa huyu nabii kijana.

58 Jinsi Mungu anavyombariki mtu ye yote atakayedumu mwaminifu katika Neno la Mungu. Naam, huenda asipendwe sana na watu, bali yeye atabarikiwa. Na sasa, watu hawana budi kujichagulia, kama wanataka kutenda kama watu wale wengine ama wanataka kubarikiwa na Mungu. Basi, waweza tu kujichagulia. Iwapo utaiishi kama wengine wao, utabarikiwa nao; bali ukielekza shauku—shauku zako zote kwa Mungu, utabarikiwa na Mungu. Kwa hivyo huna budi “Kuchagua leo ni nani utakayemtumikia,” kama alivyosema nabii. “Kila mara kumbuka Muumba wako, kwanza, siku zote.”

59 Naam, bali. . . Wakati huyu mfalme alipofikia mahali, akiwa mtu mkuu hivi na akimshawishi Isaya na watu wenye haki, bila shaka, wa ufalme wake, alifikia mahali—alijisikia kuwa salama. Na hapa ndipo unapokosea. Hapo ndipo watu wengi wenye haki huuma mavumbi ya aibu, huuma mavumbi ya kushindwa, ni kwa sababu wanaanza kujisikia wako salama. Unaanza kujisikia ya kwamba umemtumikia Kristo muda mrefu sana, ya kwamba haidhuru ataleta nini mbele yako, utajichangulia kama

unakitaka au la. Huna budi kuendelea kumtumikia Mungu. Haidhuru ulikuwa nini miaka kumi iliyopita, ni kile ulicho sasa.

⁶⁰ Mfalme huyu alifikia mahali alipowazia mwenyewe, hata akajitukuza. Majivuno yakaingia moyoni mwake. Na hivyo ndivyo inavyotendeka kwetu. Kama utaruhusu matamshi haya, hivyo ndivyo ilivyotendeka kwa makanisa yetu nchini kote. Kuna watu wazuri mle; baadhi ya watu walio bora sana duniani huenda kanisani. Nadhani walio bora zaidi ulimwenguni huenda kanisani. Bali jambo ni kwamba, utaratibu wa the—dhehebu huanza kujitukuza. Hivyo ndivyo ilivyotendeka kwa Wa—Wamethodisti; hivyo ndivyo ilivyotendeka kwa Wabatisti; hicho ndicho kilichowapata Wanazarene, Pilgrim Holiness, Wapentekoste—walijitukuza, wakaidi, kujifikiria wenyewe, hujivuna, hivi kwamba huwezi kuwaambia cho chote. Mungu hawezi kupata njia ya kuingia katika mioyo yao. Ni kwa sababu wamekuwa wajua-yote sana hata hakuna anayeweza kuwaambia cho chote. Na kwa kijiwanaja juu ya majandiliano na wandugu, wanajijenga wao wenyewe juu ya kanuni zao za imani. Na wanapofanya hivyo, wanamwacha Mungu kule nyuma.

⁶¹ Hivyo ndivyo inavyotendeka kwa madaktari. Wanapoanza kujifikiria wenyewe sana hata hawana haja na msaada wote kutoka kwa Mungu, hapo ndipo sitaki mmoja—sitaki hata mmoja wa kunichezea-chezea. Unapomwondoa Mungu katika lote, basi nawe—nataka uniondoe pia. Waona? Kwa sababu huna budi daima kumkumbuka Mungu kwanza! Yeye akajitukuza.

⁶² Watu wengi sana leo...Chukua ja—jamaa ya watu watakaoanza kuhudhuria kanisa. Naye Mungu ataponya maskini jamaa hiyo. Atawabariki, na kuwapa Roho Mtakatifu maishani mwao. Maskini watoto hao wataomba mezani; wataomba kabla hawajaenda kitandani. Mama na baba wataunganisha mikono yao na kuomba. Na mradi tu wanaendelea hivyo, watadumu kama jamaa; bali hebu waache wapate... Jambo la kwanza wajua, hawakuwa na kitu, motokaa mbovu na kuukuu, labda, wakiiendesha, labda wanaenda kwa miguu. Hatimaye wanapata motokaa nzuri, nyumba nzuri. Wanataka kuwa kile wao—ulimwengu uitacho, watu wa hali ya juu ya maisha washirikiane nao. Wanahamia ujirani, na mle ndani, wanaona ya kwamba wao wameshawishiwa na ushawishi mbaya. Inakupasa kukaa daima mahali ulipo Ufalme wa Mungu na ambapo utukufu wa Mungu unamiminika. Kaa ambapo unaweza kulishwa kiroho usiku na mchana. Kisha, punde si punde, utengano unaingia nyumbani, na kilimwengu, nao wanajitukuza. Uzia alifanya hivyo; yeye alijitukuza, kiburi kingi.

⁶³ Na sasa, tunaona yale aliyotaribu kufanya. Naam, kilichompata hasa alipojitukuza moyoni mwake (tunaambiwa katika Biblia, katika Mambo ya Nyakati 26—tunaona-2 Mambo

ya Nyakati 26), tunaona ya kwamba yeye aliingia katika hekalu la Bwana akiwa na chetezo mkononi mwake kumfukizia Bwana uvumba. Na alipofanya hivyo, yule mhudumu wa hekalu pamoja na wahudumu wengine themanini wakamfuata na kumwambia, “Usifanye hivyo; umekosea. Wewe si mhudumu. U mfalme, wala si mhudumu.”

⁶⁴ Naye akaghadhabika, akapandwa na hamaki. Basi hasira yake ilipomwondoka, akawasha chetezo kwenda popote. Naye Mungu akampiga kwa ukoma papo hapo alipokuwa amesimama pale katika hasira yake; naye akafa mwenye ukoma. Iliwabidi kumwondoa hekaluni.

⁶⁵ Hapo ndipo tunapotaka somo sasa. Kama mtu huyu ambaye Mungu alikuwa amembariki katika kazi yake. . . Bali yeye hakuridhishwa nayo, alitaka kupachukua mahali pa mtu mwingine. Hauwezi kuwa kitu. . . Kama Mjumbe wa Bunge Upshaw (mnamkumbuka, yule ambaye—ambaye alikuwa kiwete kwa miaka sitini na minane naye aliponywa mkutanoni kule, mwajua. Yeye alikuwa Mjumbe wa Bunge la Marekani.), alisema, “Huwezi kuwa kitu usicho.” Basi hiyo ni kama kweli. Huna budi kudumu katika wito wako, ambao Mungu alikuitia.

⁶⁶ Naam, mradi tu alidumu mfalme, na—alikuwa baraka kwa watu kwa kuwa mfalme. Bali alipofikiri yeye alikuwa mhuduma, basi. . . Alidhani kwa sababu Mungu alikuwa amembariki, yeye angalikuwa cho chote alichotaka kuwa. Bali alikuwa baraka kwa watu kama mfalme, bali si baraka. . . Akawa laana juu yao alipojaribu kupachukua mahali pa mhuduma. Nasi tuna watu wengi sana kama hao. Kila mtu anataka kuchukua mpira. Mwaona?

⁶⁷ Unapocheza mpira (kwa kuwa ni msimu wa kandanda), jambo tunalotaka kufanya, si kila mtu ajaribu kumnyang’anya mpira yule mtu aliye nao; ni kujaribu kumkinga huyo mtu. Mlindeni; mwache apite. Tunajaribu kuingiaza goli. Mwaona?

⁶⁸ Bali ungaliwazia timu ambayo haijapata mazoezi sana hata kumpata mtu mmoja—mtu wao—akiwa na mpira amekimbia kuingiza goli, naye badala ya kujaribu kumwondolea adui, timu ya adui, kumwacha mtu wenu aliye na mpira kuukimbiza, kila mtu anajaribu kutoa mpira mikononi mwake. Naam, hapana shaka mtashindwa.

⁶⁹ Na siku hizi, tuna jambo lile lile. Tunapomwona Mungu akijitokeza, na akibariki kitu fulani hebu na tuzuie adui kukifikia. Na tutumie ushawishi wetu kama wakinga, sio wakimbizaji, wakinga wanaomkinga anayekimbiza mpira, wamwache apite na mpira, maana hamna pingamizi, na yeyote ikupasayo kufanya ni kuendelea kukimbia. Nasi yatupasa kuwa wakinga.

⁷⁰ Mimi huzungumza kote duniani, mwajua, kwa niaba ya Wafanyi Biashara wa Injili Yote, kote ulimwenguni, nikianzisha

makundi. Na si muda mrefu uliopita ambapo, naamini, ilikuwa kule Kingston, Jamaica, walipomwalika Castro na wengine wao kule katika mkutano huu (ama tulikuwa kule kwake, hivyo ndivyo ilivyokuwa), na watu mashuhuri na wengine wote kutoka kote viziwani walikuwako kule; na hao wafanyi biashara walikuwa wakijaribu kuhubiri Injili. Yeye yuko nje ya mahali pake. Sisi wahubiri tumekuwa na shida kutosha kuiweka sawa. Nao hutumia ushawishi mdogo sana wanaoweza kuupata, na kila namna ya ustadi *huu* na *ule*, na kuitia wasiwasi sana hujui la kufanya.

⁷¹ Wakati mwingi katika—kanisani—kanisa dogo linaweza kuwa na ufufuo; mtu fulani atataka kwenda huku nje na kuongoza mkutano wa maombi. Ndiposa, yeye ana wazo tofauti na yale Biblia isemayo hasa, bali anaamini hivyo kwa vyovyote, naye atanza kuwa na ushawishi na kuwavuta wengine kutoka kwake. Jambo likupasalo kufanya ni kuukinga Ujumbe huu jinsi unavyokwenda, udumu pamoja nao, na uondoe kila kitu toka kwake, iwapo tutavuka kamwe ule mstari wa goli.

⁷² Nami nikasema, “Wandugu, kuna kasoro. Ninyi watu ni wafanyi biashara. Kwanza, hamfahamu jinsi ya kuiendea. Hamfahamu njia ya kuiendea huduma, kwa sababu huduma ni kipawa kilichoitwa na Mungu.” “Mungu ameweka katika Kanisa, wa kwanza mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, na wachungaji.” Mungu aliwaweka mle kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa. Wafanyi biashara inawapasa kushuhudia. Wanawake, mke nyumbani, haidhuru kama wewe ni yaya katika nyumba ya mtu fulani, shuhudia. Fanya yote uwezayo kwa ajili ya Ufalme; bali usithubutu kuingiza mawazo yako mwenyewe; sema tu yale Ujumbe usemayo na uzidi kuendelea (waona?), halafu basi huenda ukawa na ushawishi. Vema, usijaribu kuhubiri sasa hata Mungu, mwajua, atakapokuita. Kaa tu na huo, ushuhuda wako, kwa maana kama hufanyi hivyo, utashika njia mbaya, ndiposa utachafua kila kitu. Hivyo tu. Na haimpendezi Mungu kamwe. Hii inaithibitisha hapa.

⁷³ Wakati huyu mfalme. . . Basi, alipokaripiwa na kuambiwa iliyo kweli na yule mhudumu wa hilo jengo, na kujaribu kumwambia ya kwamba alikosea, ya kwamba Mungu aliitia hayo uzao wa Haruni, nao walikuwa wamewekwa wakfu kwa ajili ya huo utumishi pekee. . . Hayo ndiyo tu waliyowapasa kufanya, walikuwa wamewekwa wakfu kwa ajili ya hiyo. Na mfalme, haidhuru alikuwa mwenye haki vipi, ama jinsi Mungu alivyokuwa amembarikia, hakuwa na haki ya kufukiza uvumba. Alikuwa akichukua mahali pa kuhani, naye hapaswi kufanya hivyo. Naye alipokaripiwa, akaghadhibika; akapandwa na hamaki, na mara hasira yake ilipompanda, ukoma ukatokea usoni mwake. Akashikwa na ukoma, na akaangusha hicho chetezo na kufanya haraka kutoka humo jengoni. Mwaona? Kujaribu kumwigiza mtu mwingine, haitupasi kufanya hivyo.

74 Alikosea kwa hasira, naye akapigwa. Lo, bila shaka ilikuwa somo kwa huyu nabii kijana kuona hayo, sasa, haidhuru huyo mtu alikuwa mkuu vipi, ilimpasa kudumu katika wito wake.

75 Natambua ya kwamba haya yanaswa, nami najua yata—yanaenda ulimwenguni kote, kule misituni, na Wahottentoti, na kadhalika. Ujumbe huu usiku wa leo utatafsiriwa katika lugha nyingi. Bali nasema haya kwa moyo wangu wote, je. . . Watu wengi wanasema, “Mbona huungani na madhehebu fulani? Mbona usiambatane na Wapentekoste? Mbona usiambatane na kundi *hili*? Mbona usiyaachilie mambo haya madogo yaondoke?” Naweza je kufanya hivyo? Sina budi kudumu na huo Ujumbe!

76 Wakati Malaika wa Bwana alipojitokeza kule mtoni katika ile Nuru kama mnavyoona, na huku imethibitishwa na serikali na kila mahali penginepo, na sayansi—utafiti wa sayansi ya kwamba ni kweli. . . Naye akaniambia nidumu na hili Neno. Basi ningeweza je kulibadilisha na kanuni za imani? Iwapo hao watu wako kule kutenda hayo, hebu wayatende. Bali sisi tuliitwa kulihubiri Neno! Usipatane; simama kwa Neno!

77 Kwa hivyo sasa mnaona ni kwa sababu gani ni jambo la hatari kujaribu kupatana na kufanya jambo lingine, ama kujaribu kujitukuza, na kusema, “Lo, naweza kufanya *hili* na kupata fedha nyingi zaidi. Naweza kufanya *hili*, na wandugu wote watakubaliana nami.” Naweza kupatana kwa hili Neno, kisha—hata asilimia tisini na tisa ya wahudumu watabadilishwa kabisa, “Hilo ni jema, hilo ni nzuri.” Nami najua sasa, wengi wao hupiga simu. . . Ni nini? Mikate na samaki, kuona watu wakiponywa, utambuzi, na nguvu za Mungu, na kadhalika, zikidhihirishwa. Wanakuchukua kule kuwa na mikutano na kuwaingiza watu katika—makanisa yao na kadhalika; bali inapofikia kukubaliana katika Neno, wataliacha. Mwaona? Hauwezi kufanya hivyo. Kaa na Neno!

78 Basi, hili lilikuwa funzo kwa huyu nabii kijana, ya kwamba haidhuru kile alichotaribu kuwa, hana budi kudumu katika mwito wake. Lo, jamani, alijifunza ta—taratibu ya Mungu kwa mwanadamu. Taratibu ya Mungu kwa mwanaume ni kukaa mahali pake. Taratibu ya Mungu kwa wanawake ni kukaa mahali pao pia. Hauwezi kupachukua mahali pa mwanaume. Wanajiribu kufanya hivyo, bali usifanye hivyo. Mwanaume, usitwae mahali pa wanawake usivalie kama wanawake. Nanyi wanawake msivalie kama wanaume. Biblia inasema ni kosa kufanya hivyo. Biblia inasema, “Mwanamume anayevalia mavazi yampasayo mwanamuke, ni uchafu mbele za Mungu, machukizo.” Mnaona? Bali sasa ni vigumu kuwatofautisha mmoja kwa mwingine. Mnaona? Basi utafanyaje, isipokuwa kuyakemea hayo? Vema, unapofanya hivyo. . .

79 Je, uliona haya maamuzi ya mahakamani juma hili katika Indiana? Ni fedheha jinsi gani! Miaka isiyopungua kumi na

mitano iliyopita, jamaa moja hapa Port Fulton, (nafikiri baadhi ya jamaa hiyo wameketi hapa usiku wa leo) hapa Port Fulton, walimfukuza shuleni msichana mmoja mdogo kwa kuvalia suruali fupi shuleni. Na ku—juma hili wanajaribu kushtaki na kumfukuza shuleni (na walifanya hivyo), msichana mdogo aliyekataa kuvaa suruali fupi shuleni. Imekuwaje kwa taifa letu? Nilifikiri hii ilikuwa nchi ya walio huru; nilifikiri tulikuwa na haki—uhuru wa kidini.

⁸⁰ Huyo baba alisimama na kusema, “Ni kinyume cha dini yetu kwa watoto wetu kuvalia suruali fupi, msichana wetu mdogo wa miaka kumi na sita, kumi na saba, kuvalia suruali; ni kinyume cha imani yetu.” Nao wakamtoa na kumfukuza huyo mtoto shuleni.

⁸¹ Nasikia ya kwamba kila mtu ambaye hatakubali na kuingia katika—katika—mapatano ya dunia nzima ya ushirika huu wanaojaribu kuunda kuweka—na kuunganisha makanisa yote pamoja, ule muungano wa makanisa, ya kwamba wale wote ambao hawatakuja na kuungana nao, wao wanawatengenezea mkoa mdogo; watawapeleka Alaska. Afadhali basi ujitayarisha kwa hali ya baridi, maana yaonekana kama kwamba inakuja. Basi, ni fedheha jinsi gani!

⁸² Rafiki wa maisha yangu, Jim Poole, mwanawe anasimama hapa usiku wa leo. Laiti babaye angalikuja na kuona yale mwanaye aliyotenda. Nasi tulikuwa tukizungumziana leo kwa simu, naye alikuwa akinena kuhusu, naamini, mtangazaji mpya ama ye yote yule, (sikumbuki ilikuwa nani hasa), bali alisema, “Ilikuwa kwamba—kwamba Wamarekani walioga mara moja kwa juma na kuomba kila siku,” na kasema; “siku hizi wao huoga kila siku na kuomba mara moja kwa juma.” Naamini afadhali nikae bila kuoga. Bali hiyo inaonyesha tu jinsi tulivyoanguka. Imekuwaje kwa taifa hili?

⁸³ Nilikuwa Ohio yapata miaka mitano iliyopita, nami nilikuwa na mkutano kule kwenye (mahali hapo panaitwaje niliposikia habari hizo? [Mtu fulani anasema, “Chataqua”—Mh.]—Chataqua. Nami nilikuwa nikisikiliza taarifa ya habari hotelini, nayo ilisema, “Ua la uhuru lilinyauka adhuhuri ya leo mahakamani hapa Ohio.”

Wale Waamish, hawaamini katika kuwapeleka watoto wao katika shule za kawaida. Wana shule zao wenyewe. Na katika ujirani huo fulani hawa walimokuwa, hawakuwa na shule zo zote ya sekondari. Sheria za Ohio na Indiana (nafikiri ni sheria ya taifa) ni kwamba watoto wote hawana budi wawe shuleni mpaka watimie umri wa miaka kumi na sita. Na mtu huyu alikuwa na watoto wachache, msichana na mvulana, ambao hawakuwa na miaka kumi na sita; nao wakakataa kuwapeleka shuleni ambamo wanafundisha kanuni za Darwin (ya kwamba mwanadamu alitoka katika chembe chembe moja, ni nyani;

hicho ndicho aliche hasa; nyani wa hali ya juu tu na . . .) Na kwa hivyo, wao hawakukubaliana na hayo, nao hawangewaruhusu watoto wao wasikie hayo. Na kwa hivyo mahakama ikawafunga. Na huyu hakimu anayejidhanzia mwerevu sana akawaambia hawa baba na mama wazee, baba aliyekata nywele kizee na amevalia ovaroli, akasema, “Bwana, mkoa huu wa Ohio una sheria isemayo ya kwamba mtoto anapaswa kwenda shuleni hata atakapokuwa na miaka kumi na sita,” kisha kasema; “mmekataa kuwapeleka watoto wenu. Mwasemaje?”

⁸⁴ Akasema, “Bwana Mheshimiwa, naheshimu sheria za mkoa huu mzuri ambao mimi ni mwenyeji wake.” Akasema, “Bali tulikuja hapa miaka mingi iliyopita, wazee wetu, kwa ajili ya uhuru wa dini, na hiyo ndiyo sababu tuko hapa, kwa ajili ya uhuru wa dini. Dini yetu inatufundisha ya kwamba hatuamini kwamba tulitoka kwa wanyama tukawa wanadamu ambao. . . Tunaamini ya kwamba tuliumbwa katika mfano wa Mungu. Kwa hivyo, ni kinyume cha imani ya dini yetu kuwapeleka watoto wetu katika shule inayofundisha mambo kama hayo. Kwa hivyo, hatuna shule yo yote ya sekondari hapa ambayo watoto wetu wanapaswa kuhudhuria. Na hiyo si kwa sababu hatuwaheshimu ninyi; tunaheshimu mambo mnayoamini; lakini kwetu sisi, hatuamini hayo, hatutaki watoto wetu wafundishwe hayo.”

Akasema, “Au mtawapeleka watoto wenu shuleni au wewe na mke wako mtafungwa jela kwa miaka miwili.” Kasema, “Ni nini maamuzi yenu?”

Akasema, “Mimi na mama tutafungwa hiyo miaka miwili.” Nao wakageuka na kuanza kutoka nje.

Huyo hakimu hapana budi alijisikia amehukumika kidogo, kwa hivyo akasema, “Kumbukeni, si Biblia yenu husema, ‘Mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari?’”

Naye huyo mzee akageuka, akasema, “Na Mungu je, . . . ?”

Mtangazaji wa habari alisema “Vema, basi uhuru . . .”

Naye hakimu akasema, “Nawahukumieni kifungo cha miaka miwili.”

Akasema, “Hapo uhuru—lile ua la uhuru lilinyauka huko mahakamani aduhuri ya leo.”

⁸⁵ Hata hivyo, Wadunkard—ama Waamish, hasa, haidhuru wao ni wa kipekee vipi, wao wanaamini katika maisha matakatifu. Na hamna rekodi po pote Marekani ambapo wamepatikana na hatia ya watoto. Hamna hata mtu mmoja, mtoto mmoja, kutoka dini yao aliyepatwa na hatia ya watoto. Acha wawe wa kipekee wanavyotaka kuwa; wao wamelewa vyema. Siwalaumu.

⁸⁶ Bali sikizeni, lile ua la uhuru lilinyauka papo hapo, bali baada ya dakika kumi likafufuka tena. Mwakili wa mashtaka, wote, wakarudisha vitabu vyao, na kusema, “Basi tumejiuzulu

kazi zetu, kwa maana ukivunja haki hiyo ya Katiba, watavunja zilizobakia.”

⁸⁷ Uliona hivi majuzi wakati yule Askofu mzee mwenye hekima wa Kimethodisti, alivyosema kuhusu yale—kuomba yale maombi katika—katika kanisa—shuleni? Hilo halikuwa kanisa Methodisti. Huyu askofu alikuwa na hekima kutosha kujua hayo. Hilo lilikuwa kundi lingine likijaribu kuona wangeenda umbali gani kulazimisha ombi fulani shu—shuleni. Kama wanalipitisha hilo, wanalipitisha yale mengine upesi walivyoweza. Wanatafuta kila njia wawezayo. Usifadhaike, wataipata.

⁸⁸ Lo! tunataka msalaba. Tunamtaka Kristo sasa tunapoweza. Usishawishiwe na mtu ambaye labda anaweza kukupelekea chakula ki—kingi zaidi. Usishawishiwe na mtu ambaye labda atakupa motokaa bora zaidi ya kuendesha, ama nyumba nzuri ya kuishi, na kuuza haki yako ya mzaliwa wa kwanza kwa Kristo. Usifanye hivyo! Tazama unayofanya. Kila mara mfuate yule ambaye anashawishiwa na Mungu, unayejua kwamba Mungu yuko pamoja nao. Usifuate ushawishi mbaya. Naam! Vema. Usijaribu kupachukua mahali pa mwingine.

⁸⁹ Lile ono kwenye hekalu, aliona juu—juu ya kiti cha enzi Mungu ameinuliwa juu, Mungu akiwa ameinuliwa juu. Sasa mwaona, huyu mfalme ambaye... Yeye alitoa kielelezo mbele ya Isaya, naye Isaya akaona ya kwamba huyo mfalme mara tu alipoacha wito wake basi—Mungu akampiga kwa ukoma. Basi Isaya akawazia, “Yanilazimu kufanya nini?” Uzia alikuwa amekufa, alikuwa amemtegemea sana. Naye akafikiri amekwisha; angefanyaje? Maisha yenyewe yalikuwa karibu yamemwishia. Basi huyo nabii kijana alifanyaje? Akashika njia akaenda hekaluni kuomba. Akaanguka madhabahuni, akapasa sauti.

⁹⁰ Wakati mwingine Mungu huachilia hata nguzo zetu ziondolewe chini yetu. Wakati mwingine Yeye huachilia magonjwa yatupige. Huachilia machukizo, kuvunjika mioyo, kutupige. Mara kwa mara Yeye hufanya hivyo kukufikisha ambapo utashawishiwa na Injili. Uwe mwenye hekima sana kupata hayo. Usiwe mjinga hata ukayaachilia hayo.

⁹¹ Tazama, Isaya alijua ya kwamba hana budi kupata kitu tofauti. Kwa hivyo yeye alifanya nini? Akaenda hekaluni; akainua mikono yake, na kumlilia Mungu. Naye akapata ono. Na alipopata ono, alimwona Mungu, si kiti cha enzi humu chini, bali ameinuliwa juu, juu sana. Lo, jamani! pindo za vazi Lake zikimfuata na kuinuliwa juu hata Mbinguni. Naye akatazama huku na huko hekaluni, Maserafi wakiruka. Lo, jamani! *Serafi* maana yake ni “wanaowaka,” ndiyo maana ya neno *Serafi*. Ambao wako karibu na madhabahu. Kweli, Maserafi ndio wanaopokea sadaka, nao humtakasa mwabudu,

kisha wanampeleka mbele za Mungu, ndivyo Serafi afanyavyo. Basi, huyu Serafi alikuwa kiumbe cha kimalaika, nao ndio walio karibu sana na Mungu, papo hapo madhabahuni. Nao wanaipokea sadaka. Inaonyesha haki ya Mungu, ya kwamba dhambi haiwezi kuwa kwenye uwepo Wake isipokuwa iwe imelipiwa. Mwaona? Basi hawa Maserafi . . .

⁹² Mnakumbuka katika zile Nyakati Saba za Kanisa jinsi walivyozilinda zile Injili, mmoja kila upande? Mwakumbuka, tuliwarudisha kwenye bustani ya Edeni wakiwa na upanga wa moto wamesimama mle? Wao wanalinda madhabahu.

⁹³ Naye Isaya, yule nabii mkuu, alipoingia katika Roho, kwanza alimwona Mungu amesimama juu kabisa Mbinguni, juu ya kila mfalme wa duniani. Kasema, “Nalimwona *yule* Mfalme, Bwana ameketi juu sana na kuinuliwa sana (basi alimwona yule Mfalme halisi), na pindo la vazi Lake lilimfuata.”

⁹⁴ Naye akawaona Maserafi wakiruka kule jengoni. Walikuwa wamefunika nyuso zao kwa mabawa yao, mabawa juu ya miguu yao, nao waliruka kwa mabawa mawili. Nao walikuwa wakiitana, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!” Ni—ni muziki jinsi gani, ni mdundo jinsi gani! Mnasema, “Hapana budi walikuwa wakisema haya kwa sauti ndogo sana. ‘Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi.’” [Ndugu Branham anaigiza—Mh.]

⁹⁵ Isaya alisema, “Waliponena, vizingiti vya hilo jengo vilitikisika kwa sauti yao.”

⁹⁶ Hawakuwa tu wakisema sasa, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu [Ndugu Branham anaigiza—Mh.]” Lo, ni sauti jinsi gani. Kisha kasema, “Na vizingiti vikasogea na kutikisika kwa sauti zao.” Walikuwa wakipasa sauti sana, hao viumbe wa kimalaika waliosimama karibu na Mungu, wakipaza sauti, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Ni Bwana Mungu Mwenyezi!” Ni ono jinsi gani! Whiu! Lo, jamani!

⁹⁷ Tazama tena, Isaya aliyekuwa akimtegemea Uzia na akamwona akifa chini ya hukumu ya Mungu; kisha akawaona hawa viumbe watakatifu waliokuwa kando ya Mungu, wale Maserafi wakipasa sauti, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!” . . . Nao hao Malaika watakatifu walifunika nyuso zao. Malaika Watakatifu walifunika nyuso zao takatifu mbele za Mungu mtakatifu, basi sisi tu akina nani? Na sasa . . .

⁹⁸ Lo, enyi Wamethodisti, na Wabatisti, na Wapresbeteria, na Wapentekoste, sisi tu akina nani? Wakati Malaika watakatifu wanapoficha nyuso zao takatifa chini ya ubawa kusimama mbele za uwepo wa Mungu, wakati Malaika, kiumbe ambaye hakika yuko juu zaidi ya Malaika . . . Malaika hawasimami mle, ni Serafi pekee. Wao wako juu zaidi ya Malaika. Naye Mungu ni

mtakatifu sana hata wao huufunika uso wao mbele ya uwepo wa Mungu mtakatifu. Na jambo tu ambalo wangelisema lilikuwa, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Ni Bwana Mungu Mwenyezi!” Whiu! Kifuniko chao maalum wapate kusimama mbele ya uwepo wa Mungu. . . Je, sisi nasi tunahitaji kifuniko cha namna gani? Iliwabidi kufunikwa.

⁹⁹ Basi, nataka kusema hili sasa hivi: Damu ya Yesu Kristo inatosha kabisa. Mnaona? Kristo hakufa kwa ajili ya hao Maserafi. La, la! Bali wao walikuwa viumbe walioumbwa. Yeye hakuwafia Malaika kamwe; Yeye alikufa kwa ajili ya wenye dhambi. Yeye hakufa kamwe kwa ajili ya watu watakatifu; alikufa kwa ajili ya wasio watakatifu. Na mradi unafikiria eti wewe ni mtakatifu, Yeye hawezi kukufaa kitu. Bali unapotambua ya kwamba wewe si kitu, basi Yeye alikufa—alikufa kwa ajili yako. Waona? Unapotambua ya kwamba wewe si kitu, basi Yeye Ndiye—wewe ndiwe aliyekufia. Mungu ni mtakatifu kabisa. Hamna kitu kwake ila utakatifu; hivyo tu, utakatifu.

¹⁰⁰ Naam, hebu na tuone mabawa haya kwa dakika chache. Tunaona ya kwamba kwa mabawa mawili alijifunika uso wake. Jamani, waza! Hata Malaika watakatifu walizifunika nyuso zao takatifu mbele za Mungu mtakatifu. Na jambo pekee wangelisema lilikuwa “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu Bwana Mungu Mwenyezi!” Nasi tunaambiwa ya kwamba wao walilia mchana na usiku. Hiyo ndiyo hatua ya kwanza ya Mungu kushuka chini. Mchana na usiku, hamna kupumzika. Nanyi mnadhani eti tunapiga kelele sana. Wafikiriaje kuhusu mamilioni wa hao waliokizunguka kile kiti cha enzi wenye sauti iliyotikisa vile vizingiti vya hekalu wakati tu mmoja wao alilia kwa sauti, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu”? Mwajua, sauti yake ilitikisa hekalu, huku mamilioni yao wakilia karibu na kile kiti cha enzi cha Mungu. “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, Mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi,” huku wamejifunika nyuso zao kwa mabawa, mabawa juu ya miguu yao, mabawa kwa uchaji, heshima. Lo, jamani!

¹⁰¹ Sasa hamna uchaji wala heshima kwa cho chote kinenacho kuhusu utakatifu. Ukinena kuhusu utakatifu, unaitwa mtakatifu anayefingirika. Hamna uchaji, hamna heshima hata kwa Mungu, watu Wake, wala Neno Lake.

¹⁰² Naam, kundi hili litaishia wapi? (Nafikiri ulisema kweli, Ben. Ulidunda msumari kichwani wakati huo, mwanangu. Naam, hilo ni kama kweli.) Hili kundi lisilomheshimu Mungu litaishia wapi wakati huo? Hili kundi la wasio na kicho litaishia wapi (ndivyo!), wale ambao hawana heshima hata kidogo kwa Mungu.

103 Mwajua, ilikuwa kwamba kama mwanamume ama mwanamke alisema alikuwa Mkristo, watu waliheshimu hilo; bali siku hizi wao wanataka tu kuona ni mizaha kiasi gani wangepanya toka kwake. Mwaona? Kundi lisilo na kicho! Jamani! Kwa nini? Mwajua nini? Hii ndiyo sababu yake. Wao hawahisi kuwa hiyo ni Kweli. Hawamhisi Mungu. Hawakumbuki ya kwamba Biblia inasema, “Malaika za Bwana hufanya kituo, wakiwazunguka wale wamchao.” Wao hawaji tu kuwatembelea; wao—wao wanapiga hema zao. Amina! “Malaika za Bwana hufanya kituo, wakiwazunguka wale wanao licha Jina Lake.” Wao hukaa pale usiku na mchana.

Yule Ndugu mweusi mzee aliimba huo wimbo, *Malaika Hunilinda Mimi Daima*. Kasema,

Mchana kutwa usiku kucha Malaika hunilinda
daima . . .

104 Hiyo ni kweli. Mchana kutwa usiku kucha, Malaika hunilinda mimi. Yesu alisema kuwahusu wadogo hao, kasema, “Angalieni msikoseshe mmojawapo wao, kwa maana Malaika zao siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye Mbinguni.” Mwaona? Kila mara wamefanya kituo kuwazunguka, wakiwalinda hao. Nao hata hawaamini hayo, watu wasiomcha Mungu. Tutaona maana ya kumcha na kutokumcha Mungu asubuhi, Bwana akipenda.

105 Sasa tazama, wao hata hawaamini hayo. Wamepoteza adabu yote, heshima yote, uchaji wote, na hata hivyo wanaenda kanisani. Kundi lisilo na kicho kabisa, ni hao waendao kanisani. Hiyo ni kweli.

106 Maskini mtengeneza pombe, mtengeneza chang’aa, ajaye barabarani, akipita tu hapo na, ni mlevi nusu, hebu zungumza naye habari za Bwana, atasimama na kuzungumza nawe. Baadhi ya hao vidanganya macho, wanaojiita waamini, washiriki wa kanisa, watakuhekelea usoni, maana hawataki. . . ? . . . Bila shaka! Wao hawana heshima. Wadhani huna budi kuwa mfuasi wa kundi lao, au hata hutaishi wanakoishi. Waona? Ni kweli. Kutokuheshimu.

107 Basi, hawa Malaika, wanapokuwa mbele za Mungu, walikuwa. . . Waliliamini. . . Daudi alisema (mnakumbuka tulikuwa na hayo siku chache zilizopita nilipokuwa nikihubiri juu ya jambo fulani), naye akasema—Daudi akasema, “Nimemweka Bwana mbele yangu daima, kusudi nisiondoshwe. Kwa hiyo,” akasema, “Basi nikifanya hivyo, mwili wangu nao utakaa kwa kutumaini.” Naam, bwana! “Maana najua yale. . . Yeye hatakuachia kuzimu nafsi yangu, wala hatamtoa Mtakatifu Wake aone uharibifu. Kwa maana Bwana yuko mbele yangu daima.”

108 Po pote uendapo, mweke Mungu. Ikiwa mtu atakukasirikia na kukulaani wewe mweke Mungu kati yako na yeye. Ikiwa

mtu atakuita Mtakatifu anayefingirika, weka Mungu kati yako naye. Kama mkeo atakukasirikia, mweke Mungu. Mumeo akikasirika, mweke Mungu. Watoto wakikukasirisha, mweke Mungu. Waona? Cho chote utendacho, mweke Mungu. Kama baba ama mama akikupiga na kukurudi, mweke Mungu. Mnakumbuka alivyosema Mungu kuhusu hayo? “Mlee mtoto kwa njia impasayo.” Waona? Kila mara kumbuka, mweke Mungu. Mweke Mungu mbele zako, nawe utamcha Mungu na kumheshimu. Hiyo ni kweli.

109 Sasa tazama! Kwa mabawa mawili akafunika uso wake na kwa mabawa mawili. . . Hiyo ilimaanisha kicho, kuonyesha heshima mbele za Mungu, kainama—akafunika uso wake. Naam, ha—hatuna mabawa ya kufunika nyuso zetu, sisi huinamisha vichwa vyetu miguuni Mwake, tunaviinamisha vichwa vyetu na kuomba katika unyenyekevu, heshima. Naam, bwana! Mtambue. Na kwa mabawa mawili akafunika miguu yake. Miguu yake. . . Akafunika, miguu yake—iliwakilisha unyenyekevu na heshima.

110 Kama Musa, Musa katika—kumheshimu Mungu alipomwambia ya kwamba yeye alikuwa katika mahali patakatifu, akatoa viatu vyake. Waona? Akafanyia miguu yake kitu. Paulo katika kumheshimu Mungu, kicho. . . Yule Malaika wa Bwana alipomjia katika Ile Nguzo ya Moto, akaanguka chini kifudufudi. Heshima! Yohana Mbatizaji, alikuwa na heshima sana alipomwona Yesu akija, akasema, “Mimi sistahili hata kuigusa miguu Yake.” Unaona? Miguu, akitoa heshima. Waona?

111 Lo! Pata ufahamu, hapa kuna kitu kimoja tu unachopaswa kufahamu: udogo wako. Ukitaka kufikia mahali po pote na Mungu, jifanye mdogo sana. Usijikuze kama Uzia. Alifika mle, naye—yeye akasema, “Nitafanya haya kwa vyo vyote hata. . . Si kazi yako kuniambia.” Waona? Ilimpasa kujinyenyekeza. “Naam, Watumishi wa Kristo, samahani.” Hangaliambukizwa na ukoma kamwe. La! “Najua hiyo ni kazi yenu; Mungu aliwaita. Hiyo ni ofisi yenu. Haya, mkafanye hivyo, eni Mabwana. Nasikitika sasa.” Angalijiondoa, kungalikuwa na maandishi tofauti katika Kitabu hiki. Bali aliposahihishwa, akapandwa na hamaki.

112 Unaweza kuwasahihisha watu kuhusu jambo fulani ama kuwaambia kuhusu matendo yao mabaya, nao wataondoka kanisani. Wao wanataka. . . mwendee mtu fulani, waambie wanawake hawapaswi kuwa na nywele fupi, “Vema, nitaenda mahali fulani ambako wanaweza kuwa na nywele fupi”.

113 Bibi fulani alienda huku hivi majuzi. . . Nilimtuma mke wangu humu. Tulikuwa kwenye mkutano fulani; hakuwa na wakati wa kuosha nywele zake. Naye. . . Nikamwambia aende kwa mojawapo ya maduka ya kurembesha apate kuoshwa nywele zake. Akaenda kule na huyo bibi hata hakujuu jinsi ya kutengeneza nywele zake. Alizisokota-sokota tu kichwani

mwake. “Naam,” kasema, “sijasafisha kamwe nywele ya mtu ye yote—aliye na nywele ndefu.” Hakujua cho chote kuzihusu. Sijui. Lo, jamani! mwaona?

114 Hawajui hata kidogo kuhusu hiyo. Kwa nini? Ni kwa sababu ya mimbara midhaifu ambayo wamekuwa wakiketi chini yake (bila shaka!), mimbara midhaifu ambamo hawangesema Ukweli. Wao wanapatana nayo. Mwaona? Bora. . . Ingalikuwa bora kama ungaliisikia. . . Nawe ungemzungumzia mmoja wao, watainuka, na kugadhabika, na kusema, “Sitamsikiza huyo mtakatifu anayefingirika tena.” Mwaona? Endelea, Wewe Uzia. Hiyo ni kweli!

115 Ukoma, naam, afadhali ningalipata ukoma wakati wo wote kuliko ukoma wa namna hiyo; vema, huo ni ukoma wa nafsi. Mwaona? Ukienda na kuambukizwa. . . Uko papo hapo umeambukizwa tena na ukoma—dhambi, ambayo ni mbaya kuliko ukoma. Ni ukoma wa nafsi.

116 Uzia labda alienda akalala pamoja na baba zake Biblia ilisema. Kwa maana alikuwa ameokoka, ni kwamba tu alifanya kosa fulani. Bali unapofanya hivyo, na huku wajua ni kosa, basi ukoma unaambukiza nafsi yako. Na haiwezekani kuingiza nafsi ya mwenye ukoma; mwajua hayo.

Kwa hivyo basi, jifanye mdogo. Jidhilini mbele za Mungu Tambueni. Msijikuze sana na kujikweza; yachunguzeni Maandiko muone kama si kweli.

117 Nilimwambia mtu fulani si muda mrefu uliopita. . . Wao walisema, “Ndugu Branham, nasikia kuwa wewe ni wa Yesu Pekee?”

Nikasema, “Ulielewa vibaya.” Waona? Nikasema, “Mimi si wa Yesu Pekee.”

Kasema, “Vema, unabatiza katika Jina la Yesu.”

118 Nikasema, “Hiyo hainifanyi Yesu Pekee.” Nikasema, “Mafundisho ya Yesu Pekee; wao hubatiza kwa ajili ya kuzaliwa upya. Siamini hayo. Siamini eti mara tu unapobatizwa katika Jina la Yesu nafsi yako—dhambi zako; naamini Petro alisema, “Tumbuni kwanza; geukeni, mlikosa shabaha; rudini.” Tumbuni halafa muonyeshe ulimwengu ya kwamba mume—mumebatizwa. Naamini hayo. Siamini kuwa kuzaliwa mara ya pili ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Si ubatizo wa Roho Mtakatifu; ni kuzaliwa mara ya pili. Tunazaliwa kwa Damu. Chembechembe ya damu hutoka kwa—namaanisha, chembechembe hai hutoka kwa Damu. Unabatizwa na Roho Mtakatifu ukaingizwa katika mwili, bali unazaliwa kwa Damu. Bila shaka. Umezaliwa na damu ya baba yako. Mimi nimezaliwa mara ya pili kwa Damu ya Baba yangu, na Baba yako—yetu, Kristo. Naam, bwana!

119 Bali unaona, hatuamini upuzi huo. Kwa maana sisi hubatiza katika Jina la Yesu Kristo, hiyo haitufanyi Yesu Pekee; hashu. La, bwana!

120 Naam, bwana! Musa alijidhili katika huo uwepo aliposikia hiyo sauti ya Mungu ikija hivyo, kasema, “Toa viatu vyako.” Musa akainama chini na kutoa viatu vyake haraka. Mwaona? Hiyo ni kweli.

121 Paulo, wakati hiyo Nuru ilipomwangusha chini... Yeye alisema, “Sauli, Sauli, mbona waniudhi?”

Kasema, “Bwana, U nani Wewe?” Mwaona, moja kwa moja chini. “Ni nani?”

Kasema, “Mimi Ndimi Yesu (Ile Nguzo ya Moto)—Mimi Ndimi Yesu. Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo.”

Kasema, “Bwana, nifanye nini?” Yeye alikuwa tayari.

122 Yohana Mbatizaji alimwona akija. Mmoja wa watu mashuhuri sana, Yesu alisema, “Hajatokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kama Yohana.” Naye Yohana alipomwona, akajitambua ya kwamba alikuwa mdogo sana, akasema, “Mimi sistahili kumvua viatu Vyake.” Amina!

123 Kila mara angalieni, mtu aliye mkuu hujidhili mwenyewe. Njia ya kupanda juu ni kushuka, kila mara. Jifanye mdogo, naye Mungu atakuinua. “Kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa.” Lo, jamani, napenda hayo.

124 Jifanye mdogo; mdogo daima. Usiwe bwana mkubwa; kuwa mtu mdogo. Waona? Mungu ndiye tu kati yetu aliye mkubwa kwa vyo vyote. Hiyo ni kweli.

125 Hutaki kusema, “Ni kanisa takatifu, ni watu watakatifu.” Lo, sivvo! Ni Mungu mtakatifu (hiyo ni kweli) na kanisa lisilo takatifu pamoja na watu wasio watakatifu. Hiyo ni kweli. Hamna kitu kama kanisa takatifu; ni Mungu mtakatifu Kanisani. Si watu watakatifu; ni Roho Mtakatifu katika watu. Ndipo unazungumza si juu ya watu; unazungumza juu ya Roho Mtakatifu ambaye yumo katika watu. Amina, naam bwana! Hilo ndilo neno halisi! Amina! Hilo limeingia ndani; nalisikia hilo! Naam, bwana! Yeye alipenda hilo; najua hivyo. Utukufu! Naam, bwana! Vema.

126 Jifanye mdogo. Yeye alifunika uso wake kwa mawili, uchaji. Alijidhili kwa kuifunika miguu yake. Sasa ya tatu, kwa mawili akaruka. Yeye akaanza kufanya kitendo kwa mawili ya hayo. Yeye alikuwa na uchaji mbele za Mungu. Alijidhili mbele za Mungu. Si hivyo tu, yeye hakuketi tu pale, bali akafanya kitendo. Nena kuhusu Kanisa. Amina! Akafanya kitendo. Cho chote alichokuwa nacho, alikuwa tayari kwenda nacho. Naam, bwana! Jambo tu ambalo angalisema lilikuwa, “Mtakatifu, mtakatifu mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenyezi,” bali akaanza kufanya kitendo kwake. Hiyo ni kweli! Akaanza kutenda kitendo. Hilo

ndilo kanisa linalohitaji usiku wa leo, ni kwanza kuwa na kicho, jambo la pili, kujidhili, halafu fanya kitendo. Naam, bwana!

¹²⁷ Yeye alimwonyesha nabii... Alipomwonyesha nabii jinsi alivyowawakilisha watumishi Wake, jinsi angalifanya, huyu mtu alifanyaje, Malaika huyu? Huyu nabii aliona sauti yake ikitikisa vile vizingiti hekaluni alipopasa sauti. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi.” Nalo jengo likatikisika, na... Akapasa sauti teno, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi,” nalo jengo likatikisika.

¹²⁸ Isaya alisema, “Ole wangu!” Nabii, nabii aliyethibitishwa, aliyezaliwa nabii, yule nabii mkuu wa Biblia; naye akasema, “Ole wangu! kwa sababu macho yangu yameuona utukufu wa Mungu.” Mtazame huyo nabii akijidhili, nabii, mtu ambaye Neno la Mungu lilimjilia. Bali alipoona ono likitenda kitendo, yeye alisema, “Ole wangu, kwa sababu ninasimama karibu sana hata nauona Uwepo wa Bwana.”

¹²⁹ Watu wetu Wamarekani wa kisasa wanaweza kuona hayo yakitendeka, na kuondoka, na kuyachekelea. Hiyo ni kweli.

¹³⁰ Alipoona ono limedhihirishwa, ono lililodhihirishwa (ee Mungu, urehemu ulimwengu huu wenye dhambi!)—ono lililodhihirishwa, akalia kwa sauti kuu, “Ole wangu, kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu. Nimepotea kabisa; hamna neno nzuri kwangu.”

¹³¹ Vema, unasema, “Mungu abarikiwe, mimi ni Mpresbeteria, Mmethodisti, Mbatisti, Mpetekoste; hainipasi kuketi na kusikiza upuzi kama huo.” Mna tofauti jinsi gani, tofauti jinsi gani.

¹³² Nanyi mwakumbuka, huyu nabii, aliyelitwa tangu kuzaliwa kwake, na akathibitishwa, akachaguliwa tangu awali kwa kazi yake, naye alikuwa akitafuta Ukweli, naye alikuwa pamoja na mfalme. Aliziona kazi za Mungu zimedhihirishwa, bali wakati ono wazi lilipotokea, badala ya kujikweza, akasema, “Ole wangu. Nimepotea. Nitajuta, kwa sababu macho yangu yameona utukufu wa Mungu.”

¹³³ Nasi tunaweza kuona utukufu wa Mungu, na tutaenda huku na huko na kusema, “Kundi la watakatifu wanaofingirika, watu wenda wazimu.” Si ajabu hatufikii po pote.

¹³⁴ Sasa kumbukeni, naliwaambieni nilishuka kuja humu kuwaambieni jambo fulani, litakalawasaidia watu. Naam, hatuna budi kuwa—kuliheshimu. Hatuna budi kulipa heshima yote tuwezayo, tunapoona ono waziwazi kutoka kwa Mungu likinena, na kujua ya kwamba ni Kweli.

¹³⁵ “Ole wangu,” kasema Isaya. “Mimi nimo jengoni humu usiku wa leo (ama leo ama wakati wo wote ule), nami naona utukufu wa Mungu. Namwona Malaika akizungumza, nami naona kitu fulani kikijongelea. Nami natazama kule juu, na kuona Mungu

amedhihirishwa papa hapa. Ole wangu, kwa maana mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wachafu.”

¹³⁶ Tazama yaliyotendeka. Lo, Yeye alifanyaje? Alimwonyesha na—nabii Isaya ya kwamba mwanadamu atakuwa mwenye heshima, atakuwa mnyenyekevu mbele Zake. Mnyenyekevu, mwenye kujidhili, kisha kufanya kitendo. Hiyo ni kweli. Anza kufanya kitendo.

¹³⁷ Kama yule mwanamke kisimani, alipoona jambo fulani likitendeka, ndugu, alikuwa na mabawa mawili. Aliondoka kwayo upesi sana. Alikuwa kule kwenye kisima cha Yakobo chenye maji machafu waliyokuwa wakibishania; bali alipopata kinywaji kutoka kwa huo Msingi wa Uzima, akaanza kutenda upesi sana. Yeye hakusema, “Bwana, tafadhali niambie ulikopata elimu yako wapi. Ulipata wapi hayo? Ulijuaje?” ama, “Unajuaje ya kwamba nina waume watano? Ulijuaje makosa yangu? Ulijuaje nilikuwa mwanamke Msamaria? Ulijuaje mambo haya?” Yeye hakuswali; alisema, “Bwana, naona ya kuwa u Nabii. Tunajua Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya.” Jamani! Yeye alitambua hayo kwa Maandiko. Kisha akasema, “Najua Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya.”

Yeye akasema, “Mimi Ndiye.”

¹³⁸ Akaanza kitendo. Akaenda moja kwa moja mjini upesi alivyoweza; kasema, “Njoooni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je! haiyamkini huyu kuwa ndiye Masihi!” Yeye alipoona Ukweli, hakujaribu kuchukua mpira, yeye—lakini yeye bila shaka alikuwa akiupa he—he—heshima sana. Bila shaka alikuwa akiuunga mkono sana, maana alishuka akaenda mjini akisema, “Enyi, njoooni mtazame. Kama hamuamini, njoooni, muende pamoja nami.” Utukufu!

¹³⁹ Najisikia kama mtakatifu anayefingirika usiku wa leo. Naam, bwana! Jamani, kama hivyo ndivyo unavyojisikia ukiwa mtakatifu anayefingirika, hebu niwe mmoja. Naam, bwana! Najua yeye ni wa kweli. Najua Yeye yuko hapa. Najua Masihi yuyo huyo, najua Mungu yuyo huyo, Kristo yuyo huyo, yuko mumu humu katika hili jengo ndogo lenye joto usiku wa leo. Naweza kuwathibitishia. Amina!

¹⁴⁰ Mtazame yule Malaika wa Bwana amesimama pale pembeni juu ya yule mtu anayeketi hapo. Jina lake ni . . . Yeye ni kasisi. Bw. Witt. Yeye anatoka Virginia (sawa!) ana ugonjwa wa neva. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda nyumbani ukaponywe. Unaamini hayo, bwana? Vema, nenda nyumbani ukaponywe; ugonjwa wako wa neva umekwisha.

¹⁴¹ Hiyo ni kweli. Anayeketi papo hapo; jina lake ni Morriah. Anatoka Illinois. Yuna shida za utumbo. Kama utaamini hilo, bwana . . . Unaamini? Mimi ni mgeni kwako. Unaamini hilo? Utaondoka. Haleluiya!

Kaa la moto lilipomgusa nabii,
 Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo kuwa;
 Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani
 atakayekwenda kwa ajili yetu?”
 Ndipo alijibu, “Mimi hapa; nitume mimi!”

¹⁴² Haidhuru mateso ni nini, haidhuru msalaba ni nini, “Nitume mimi, Bwana; mimi hapa!” Haidhuru ni wangapi wanaokukataa, ni wa ngapi *hivi, vile*, au *vinginevyo*, “Nitume mimi!”

¹⁴³ Yeye Ndiye Masihi yule yule. Yeye yuko papa hapa sasa. Namwona tena. Amina! Ni nini?

¹⁴⁴ Huyu mwanamke akaanza kutenda kitendo. Akayashika hayo mabawa akaanza kuruka. Akaanza kutenda kitendo upesi sana.

¹⁴⁵ Wakati mtume Petro, alipolitii Neno la Mungu siku moja kule baharini. . . Alikuwa amevua usiku kucha asipate kitu. Naye Yesu akamjia; Akasema, “Litupe jarife lako upande mwingine wa chombo.”

¹⁴⁶ Yeye akasema, “Bwana, mimi ni mvua samaki; najua wakati wanapouma na wakati hawaumi. Najua waliko na ambapo hawako. Bali nimevua usiku kucha na hata sijapata samaki mdogo. Naam, ukisema nilitupe. . . Najua hamna samaki mle, bali kwa Neno Lako, Bwana, nitalitupa jarife.” Alifanyaje? Akaanza kufanya kitendo. Amina!

¹⁴⁷ Kuna kidimbwi kilichojaa maji hapa. Iwapo haujabatizwa kamwe katika Jina la Yesu, ni wakati wa kafanya kitendo. Iwapo wewe ni mfuasi tu wa kanisa na haumjui Mungu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni wakati wa kutenda kitendo. Sivyoy? Funika uso wako kwa heshima. Funika miguu yako kwa unyenyekevu, ukainamishe magoti yako uanze kutenda kitendo. Iwapo haumjui Mungu, anza kitendo.

¹⁴⁸ Wakati yule kipofu ambaye hangeweza kuona, Yesu aliponena naye, akatema mate kwenye matope, na akampaka machoni mwake, kisha akapo—akapona. Alipopona, akaanza kitendo. Akaeneza sifa Zake. Hakujaribu kubeba mpira; bali ndugu, yeye alieneza sifa Zake kote sehemu za kando kando. Alifanyaje? Akaanza kitendo.

Wakati mmoja kipofu mmoja aliponywa kisha akasema. . . “Mtu huyo ni mwenye dhambi; hata haumjui!”

¹⁴⁹ Akasema, “Kwamba Yeye ni mwenye dhambi au la, sijui; bali najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sas150aona.” Alifanyaje? Akaanza kitendo.

¹⁵⁰ Hiyo ndiyo kanisa linahitaji. Anzeni kitendo. Tuna utaratibu mwingi sana, tuna heshima nyingi sana za kilimwengu;

inatupasa kuanza kitendo. Amina! Yeye alieneza sifa Zake kila mahali.

¹⁵¹ Watu kule Pentekoste, hawakujua mengi sana. Hawangaliandika majina yao, wengine wao. Walishikwa na woga. Wakaingia orofani. Bali siku moja walifanyaje? Walipanda kule kwa kulitii Neno Lake. Walishika Neno Lake. Lo, laiti watu siku hizi wangelishika Neno Lake, basi wataanza kutenda kitendo. “Kaeni humu mjini Yerusalemu.” Luka 24:49.

“Mtapokea Roho Makatifu baada ya hii ahadi—akiisha kuwa ilia juu yenu Roho Mtakatifu; kisha mtakuwa mashahidi Wangu.” Matendo 1:8.

¹⁵² Luka 24:49 ilisema, “Tazama, nawaletoa juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini ngojeni humu mjini Yerusalemu, hata mvikwe uwezo utokao juu.” Muda gani? Saa moja, masaa mawili, siku kumi, miezi minne, miezi sita, haikuleta tofauti yo yote. Hata! Ni muda gani huo? Hata tu. Ukimwomba Mungu cho chote, kaa papo hapo hata. Amina! Najisikia vizuri. Kaa hata. Mpaka nini? Hata itimie. Idai! Iamini! Ishikilie! Tenda kitendo! Shuhudia juu yake! Shuhudia! Usiwe na hofu. Tenda kitendo.

¹⁵³ Walikuwa orofani kwa nini? Wakisifu na kumbariki Mungu. Kwa nini? Walijua ahadi ingetimia. Ndiyo hiyo; anza kitendo. Endelea kumsifu Mungu hata hiyo Ahadi itakapotimizwa. Una ahadi.

¹⁵⁴ Kama unaamini ya kwamba Mungu huponya, fanya kitendo. Kama unaamini atakuita sasa, nawe unajishikilia Kwake, fanya kitendo. Dumu kwa kitendo! Una mabawa mawili, basi yatumie. Endelea kufanya kitendo. Yapigapige mbele nyuma. “Bwana, naamini; Bwana, naamini.” Huwezi tu kupaza sauti, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu”; yakupasa kusema, “Bwana, naamini!” Dumu kitendoni! Amina!

¹⁵⁵ Waliendelea kudumu kitendoni hata ukaja uvumi kutoka Mbinguni kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi. Ndipo basi tendo likatendeka kweli. Basi wakaingia kitendoni.

¹⁵⁶ Ndugu, Dada, yale tumeona yakitendeka katika siku hizi za mwisho yanapaswa kutufanya tutende kitendo. Amina! Tunapaswa kutenda kitendo. Hiyo ni kweli hasa. Tunaketi kitako kana kwamba ilikuwa kitu fulani. . . Vema, basi, watu wanaketi kitako, Wapentekoste; Bwana atatekeleza jambo fulani; wao wakasema, “Um! Hilo ni jema kabisa.” Lo, jamani! Hawaonekani sana kama Serafi anayeishi karibu sana na Mungu. Hiyo ni kweli. Mjumbe ambaye hasa yuko karibu sana na Mungu. Unakuwa mtoto Wake mbele zaidi ya yale madhabahu ya shaba.

¹⁵⁷ Maserafi wako kwenye madhabahu ya shaba. Bali wewe kama mwana na binti huenda hata kwenye uwepo wa Mungu. Haupaswi kupitia kwa kuhani ye yote na mambo haya yote. Yeye ni Kuhani wako. Waona? Papo hapo katika uwepo Wake kama

wana na binti. Ndugu, naamini tuna zaidi ya mabawa mawili. Amina! Tuna Roho Mtakatifu! Hiyo ni kweli.

¹⁵⁸ Bali tunapaswa kutenda kitendo kwa uchaji na unyenyekevu, si katika kitendo cha kujaribu kumsukumia mtu fulani kitu fulani, bali kwa uchaji na unyenyekevu tupate kuigua kwa kitendo na kusema, “Ole wetu, tumeuona Uwepo wa Mwenyezi. Tumeona maono yakitendeka jinsi tu alivyosema. ‘Kazi nizifanyazo Mimi, nanyi mtazifanya. Naam, na kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.’”

¹⁵⁹ Tumeona mengi zaidi yakitendeka kuliko yaliyoandikwa katika... Verna, tumeona mengi zaidi yakitendeka katika mkutano mmoja wa mambo hayo kuliko yaliyoandikwa katika Biblia. Hiyo ni kweli. Mengi zaidi katika mkutano mmoja kuliko yaliyoandikwa katika ile miaka thelathini na tatu unusu ya maisha Yake. Hiyo ni kweli. Wazia hilo. Tumeona kwa macho yetu wenyewe. Tumeona ikitendeka. Tumeona ikitabiriwa, inatimia, itazame. Viwete, vipofu, walemavu, wasiojiweza, mambo yaliyotabiriwa ambayo yalitendeka vivyo hivyo. Haijakosa kutimia. Ndugu, hilo linapaswa kutuweka kwa kitendo kwa unyenyekevu na kicho.

¹⁶⁰ Tangu kule nyuma kabisa katika nyakati za Biblia wakati ile Nguzo ya Moto iliponing’inia juu ya Israeli, na ilifanyika mwili ikakaa kwetu... “Nalitoka kwa Mungu na ninarudi kwa Mungu.” Mt. Paulo aliiona naye akaanguka kifudifudi. Mwalimu mkuu kama Paulo, aliyefunzwa chini ya Gamalieli, aligaagaa mavumbini na kulia, “Bwana, Bwana, U nani Wewe? Mimi ni tayari kwenda.” Alikuwa mtu mkuu, na ni mwanachuoni; naye akajinyenyekeza, kwa sababu aliona ile Nguzo ya Moto. Hatuioni tu kwa macho yetu ikenenda kati yetu, bali tumeipata kisayansi. Hiyo inapaswa kutufanya tutende kitendo.

¹⁶¹ Tunaiona ikifanya mambo yale yale iliyofanya kule nyuma. Ingali inafanya hayo leo. Ile ahadi ya Baba. Jamani, ni nini? Inakuja kuthibitisha Neno, kuthibitisha ya kwamba Neno liko hivyo. Hilo linapaswa kulifanya Kanisa kufanya kitendo, si mwafikiri hivyo?

¹⁶² Kwa mawili akaufunika uso wake katika uchaji. Kwa mawili akafunika miguu yake, unyenyekevu. Na kwa mawili akaanza kazi. Akaondoka, akaanza kitendo.

¹⁶³ Naam, inatupasa kuwa katika kitendo kwa ajili ya Neno. Inatupasa kuwa tukiwaambia watu.

¹⁶⁴ Ishara za kuja Kwake zinaonekana, kila mahali tunaona zikijitokeza kwa Neno. Tunamsikia Roho Mtakatifu akija na kutuambia mambo fulani yanayokaribia kutendeka.

¹⁶⁵ Haijapata miaka ishirini iliyopita kutoka kwenye jengo lili hili, alitabiri kuhusu kuja kwa Rais Kennedy. Alitabiri hasa yale yangetokea, ya kwamba wanawake na kadhalika

wangemchagua mtu huyu, na yale hasa ambayo angekuwa. Tulijua hayo wakati huu wote, na mkaambiwa yale hasa yangetendeka. Na ndiyo haya leo. Na ndio huu mkutano unaokuja, Muungano wa Makanisa na wote wakiunganika. Naam, inapasa kutufanya tutende kitendo. Hiyo ni kweli. A-haa!

¹⁶⁶ Neno kwa neno kama Yeye alivyonena, inatimizwa karibu nasi hasa. Inapaswa kutufanya tutende kitendo.

¹⁶⁷ Kama yule nabii, tumeona matokeo au ku—kuja kwa kule kuondoka, kanusho, kujikweza kwa madhehebu, yakipoteza mahali pao.

¹⁶⁸ Kama vile Isaya aliposimama pale, alikuwa mtu wa—wa kidhehebu kwanza. Alimtegemia mfalme, kwa sababu alikuwa mtu mzuri. Bali aliona yale kujitukuza kulimfanyia. Kulimwondolea mbali milele. Nasi tumeona yale kujitukuza kwa kidhehebu kumelifanyia kanisa. Kumeliondoa kanisa lijiitalo la kidhehebu mashindanoni milele. Niambie wakati moja liliinuka baada ya kuanguka. Liko wapi? Tazama nyuma katika historia na uone kanisa lo lote lililowahi kuanguka. Mara lilipounda dhehebu, lilianguka, na halikuinuka tena kamwe. Uzia hakurudi he—hekaluni tena. Alikuwa mwenye ukoma siku zote zilizobakia na alizikwa mwenye ukoma. Naam, bwana!

¹⁶⁹ Sasa, huyo nabii aliona kile kilichofanywa na hayo. Aliona yale—yale huko kujitukuza kulifanya. “Kwa nini, sisi ni . . .” ama, “Karibu kila . . . Hamna mtu anayeweza kuingia katika dhehebu letu isipokuwa a—afanyiwe uchunguzi na daktari wa mawazo kuona kama akili zake ni timamu ama la. Hana budi kuwa na D.D.D., Ph.D. kabla hata hajaja ku—kunena nasi. Halmashauri zetu hazitamkubali kama hana.” Lo, jamani! “Umati . . . umati ulio bora sana nchini huhudhuria . . . Tazama motokaa zinazozunguka kwetu; ni za aina ya Cadillac, na Rickenbackers, na kadhalika.”

¹⁷⁰ Tumeona kitu hicho kikifa. Tumekiona kifu, na kitu chote kimejaa—kuhesabiwa—vindonda vilivyofanywa—vindonda vilivyooza, hasa, kama Biblia iviitavyo. Yote yameoza kabisa. Kinanuka. Hiyo ni kweli. (Kusema kiroho ninalinena. Mwaona?)

¹⁷¹ Tunawaona wakilegeza kushikilia kwao—juu ya Neno la Mungu na kuinua kanuni za imani. Tunalionga likifanya nini? Limepigwa kwa ukoma, kutokuamini. Ha! Lo, jamani jamani!

Kama Uzia alivyojaribu kupachukua mahali pa mpakwa mafuta—pa huduma iliyotiwa mafuta baada ya kupigwa, naye akaona ya kwamba alikuwa ameikosesha. Nasi tumeyaona makanisa yakijaribu kupachukua mahali pa huduma iliyotiwa mafuta kuhubiri Neno la Mungu na kupumbazwa nalo. Hawajui wafanyeje. Weka Neno mbele yao, hawajui la kufanya. Ni, lo, “Tunaamini hilo lilikuwa la siku nyingine.” Ni nini? Wametatanishwa. Waweza je kushikilia huduma ya mtiwa

mafuta wa Mungu na kukana Neno Lake lililotiwa mafuta ambalo ni Yeye katika umbo la Neno? Wawezaje kukana kwamba Neno ni kweli kisha uzidi kusema ya kwamba una upuko wa Roho?

¹⁷² Kitu pekee kitakachodhihirisha Neno La Mungu ni Roho Mtakatifu Mwenyewe. “Roho Mtakatifu atakapokuja, atachukua mambo haya yaliyo yangu na kuwaonyesheni nyinyi.” Hiyo ni kweli. Wawezaje kupachukua mahali pa huduma iliyotiwa mafuta na kuwa mfuasi wa kanuni za imani ama dhehebu? Hayo yamekufa! Jambo upaswalo kufanya ni kuanguka chini na kulia, “Bwana Mungu, mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Naam, bwana!

¹⁷³ Hayo madhehebu hujaribu kupachukua mahali pa kanisa takatifu. “Tunaamini katika Mungu Baba, Mwenyezi, Muumba wa Mbingu na nchi, na Yesu Kristo mwanawe. Tunaamini katika Kanisa katolika la Kirumi,” na mambo hayo yote mbali mbali. “Tunaamini katika ushirika wa watakatifu.”

¹⁷⁴ Naamini ushirika wa Kristo. Naam, bwana! Naamini watakatifu wako utukufuni, bila shaka. Nami naamini ya kwamba tuna Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu. Naam, bwana! Sukumiza kitu hicho... Hapa, Biblia hupinga hayo. Wao husema, “Vema hiyo ni Biblia.” Huyu ni Mungu! Neno lilikuwa Mungu, nalo Neno likafanyika mwili likakaa kwetu. Sasa, Neno limo miilini mwetu, likijidhihirisha Lenyewe, limetiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Ni wakati wa kuanza kitendo. Hiyo ni kweli.

¹⁷⁵ Matokeo ya hilo ono kwa nabii (lo, jamani!) yalimfanya aungame ya kwamba yeye alikuwa mwenye dhambi (nabii aliyetiwa mafuta.) Alisema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nimekosea. Nimetenda mabaya. Mimi mwenyewe ni mchafu.” Alikuwa mwenye dhambi. Alitubu dhambi zake. Naam, bwana! Ilimfanya nabii wa Mungu kutubu ya kwamba ni mwenye dhambi; haya ndiyo lile ono liliyofanya. Baadhi ya D.D.D., Ph.D. watachekelea hilo. Wanadhaminiwa kuwa serikali ya kanisa fulani.

¹⁷⁶ Je ulisikia aliyosema Kardinali katika ile taarifa ya habari leo? Alisema, “Kuna wengine ambao wanafundisha ya kwamba kuja kwa Bwana ku karibu.” Anasema, “Lakini bila shaka, itatupasa kuliondolea mbali kundi hilo. Tunataka kuunganisha dini za ulimwengu.” Hivyo hasa. Enyi watu, msilale sasa. Jambo hilo limekaribia kuliko mnavyodhania. Mtu huyu ni karibu kuwa kama yule asiyemjua Yusufu, mwajua.

¹⁷⁷ Tazama, aliingia kwa hila sana kama iwezavyo kuwa. Wameshikilia papa hapa mahali hapo pa mwisho, ambapo watamfanyia sanamu kwa kuchukua Muungano wa Makanisa, na kuifanya izungumze tu kama yule mnyama alivyofanya, na kuupa mamlaka kuwatesa watu wote wanaomcha Mungu,

na atabadili majira na amri za Mungu. Jinsi hasa ilivyosema. Tutafikia hayo baadaye; tumechelewa sana usiku wa leo, bali tuta—mwajua hayo kwa vyo vyote. Naam, bwana!

¹⁷⁸ Yalimfanya—yalimfanya atubu ya kwamba yeye ni mwenye dhambi...? ... Kwani, kama ingalikuwa wanaojigamba siku hizi, wangesema, “Vema, mimi ni Daktari *Fulani*.”

Nalimsikia askofu akisema, “Nitakapofika mbinguni, mnajua nitafanyaje?” Kasema, “Nitamwendea Ye—Yesu na kusema, “Wajua mimi ni nani? Mimi ni Askofu *Fulani*.”

Akasema, “Naam, nimemsikia mama yangu akinena habari zako.”

Kasema, “Watu wanaoamini Biblia ni kama wajikokotao kupitia maji yenye matope; hamjui muendako.”

¹⁷⁹ Msiwazie hayo. Yeye ni Kiongozi wangu. (Nitahubiri juu ya hilo kesho usiku.) Naam, bwana! Atakuongoza kote kwenye maji yenye matope unayopaswa kuyapitia, maji hatari, yasiyo na kina, mahali pote pa juu, na mabondeni. Po pote pale, Yeye ataniongoza juu ya mto wa mauti. Amina! Lo, naam bwana! Ataongoza. “Mauti yajapo sitaogopa mabaya kwa kuwa Wewe u pamoja nami. Naam, nijapopitia kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; Wewe uko humo.”

¹⁸⁰ “Ningefanya kuzimu kitanda changu,” Daudi alisema, “ndiye huyo pale.” “Lo, nijapochukua mabawa asubuhi, na kuruka mbali, Ndiye huyo pale. Yeye yuko mbele yangu daima, kwa hivyo sitaondoshwa.” Amina! Lo, jamani! Yachukue haya mabawa uanze kitendo sasa. Naam, bwana!

¹⁸¹ Huyu nabii alianza kitendo upesi pia; alipiga magoti. Naye akasema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Kisha mara alipoungama, basi ukaja utakaso. Huna budi kuungama kwanza.

¹⁸² Nataka uone, wakati huyu nabii... Wazia hilo, si... Mtu aliyesimama na serikali kuu, nabii aliyethibitishwa, na mara alipoona hilo ono la kwanza... Hakuwa ameona maono hapo mbeleni; alikuwa na njia zingine. Yeye alisikia uongozi wa Mungu akaenda kulingana na Neno. Bali wakati huu lilikuwa ono dhahiri, naye akapaza sauti, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu nami—watu hawa wote ni wachafu. Ole wangu, kwa kuwa nimeona utukufu wa Mungu ukidhihirishwa.” Nasi tuutazame tu. Inatupasa tuwe tukiruka mbali. Mnaona, mnaona?

¹⁸³ “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Akashuka akaenda madhabahuni, naye akasema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, Bwana. Nifanyeje, nifanyeje, kwa maana nimekuona Wewe ukidhihirishwa papa hapa? Namwona Malaika akitikisa kitu hicho. Nalimwona akinena, na kitu fulani kikarudi nyuma

kule.” Amina! (Natumaini hamjalala.) Lo, jamani! Akanena na kitu fulani kikatendeka. Utukufu! Nini kilichotendeka?

¹⁸⁴ Kisha tunaona ya kwamba yeye aliungama dhambi zake, na mara tu alipofanya hivyo, akanyosha mkono wake, akatwaa koleo, akachukua kaa la moto, hii sauti kuu ambayo ilikuwa ikinene ikaruka chini, katwaa mkononi mwake, akaja akaliweka midomoni mwa Isaya, na kumtakasa.

¹⁸⁵ Tazama, yeye hakumtuma kamwe kupata shahada ya Ph.D. Hakumpa kamwe kitabu cha sheria akajifunze; bali Yeye—Mungu alikuwa akimwonyesha huyo nabii ya kwamba nguvu Zake za utakaso ni kwa moto kutoka madhabahuni. Amina! Nguvu za Mungu za utakaso siku hizi si kwa kukariri kanuni za imani ama kujiunga na kanisa fulani; ni nguvu za Roho Mtakatifu na moto unaoshuka na kumtakasa mwanadamu kutoka kutokuamini kwote. Amina!

¹⁸⁶ Njia ya Mungu ya kumtakasa nabii ni kwa moto, si kwa kanuni za imani. Nabii angejua nini kuhusu kanuni za imani? Anaenda kutumiwa na Mungu. Neno lilikuwa laenda kudhihirishwa kupitia kwake, kwa hivyo hangalimpa kanuni za imani. Yeye angekuwa akishikilia kanuni hizo za imani. Kwa hivyo akatoa moto madhabahuni na kumtakasa nabii.

¹⁸⁷ Kuungama kwanza, kisha kutakaswa kwa moto. Utukufu kwa Mungu! Lo, tazama! Kuungama, kwanza, kutakaswa, pili, agizo, tatu. Amina! Ndiyo hayo. Kwanza kuungama, “Nimekosea!” Pili, kutakaswa. Kuhesabiwa Haki, Kutakaswa, na Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mwaona? Kuungama, kutakaswa, kuagizwa. “Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Amina!

¹⁸⁸ Baada ya maungamo huja utakaso. Baada ya utakaso huja agizo. Hubiri Injili, ponya wagonjwa. Haidhuru watu walisema nini.

¹⁸⁹ Hatimaye maskini nabii huyo mpendwa akafa chini ya mateso kwa kukatwa vipande-vipande kwa msumeno.

¹⁹⁰ Kumbukeni, ilikuwa wakati Isaya alipoungama kwamba alikuwa amekosea. Alikuwa amekosea kabisa; alikuwa akiegemea kwenye kanuni zake za imani (mwaona?), akiegemea juu ya—huyo mtu, jambo la kubuniwa na binadamu. Aliisha kumwona mfalme aliyekuwa mtu mashuhuri; alikuwa mtu wa kidini. Bali akaona ya kwamba watu wote watashindwa. Mwaona? Bali alipobadili hayo, na kutazama humu, na kuona ono kwamba Mungu alikuwa Nani, basi akasema, “Nataka kutubu ya kwamba nimekosea. Zile kanuni za imani za kale hazitafaa tena, maana zimekwisha na kufa na kushindwa. (Mwaona?) Zimepigwa kwa ukoma, bali nimekwisha kuona utukufu wa Mungu umedhihirishwa.” Kanuni za imani haziwezi kudhihirisha hilo. Kanuni za imani haziwezi kusema hivyo

Kanuni za imani haziwezi kuifanya vivyo hivyo. Inachukua Kristo kuifanya hivyo. Na mara alipoona hivyo, akasema, “Naam, nimekosea kabisa, Bwana.” Kisha utakaso ukaja; halafu agizo likaja. Lo, jamani!

¹⁹¹ Hapo ndipo basi Isaya aliyetakasika . . . Mungu alipoitana, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yangu,” na ilikuwa Isaya aliyesema, “Bwana, mimi hapa; nitume mimi!” Nabii aliyetakaswa.

¹⁹² Lo hamuoni *Ushawishi?* Usichukue ushawishi wa Marthela. (Natumaini hilo si jina humu.) Usichukue majina ya—ya—ushawishi wa msichana fulani mdogo mnayekwenda pamoja katika shule ya sekondari, ama shule ya msingi, ama jirani wa karibu anayekata nywele zake na kuvalia suruali fupi; usichukue huo ushawishi. Usichukue ushawishi wa mchungaji mwenye kanuni za imani na ambaye angekana Neno la Mungu na kukupa kanuni za imani; usichukue ushawi huo. Bali simama hapo hata utakapouona utukufu wa Mungu ukishuka, uone kitu fulani kikienenda kwa na matokeo yake, na uone ikitendeka jinsi tu Mungu alivyosema. Kisha ukalie, “Ole wangu, Bwana; nimekua makosani. Nitakase sasa, Bwana. Nitakase! Roho wa Mungu Aliye Hai shuka upya juu yangu.”

Kaa la Moto lilipomgusa nabii,
Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo kuwa,
Sauti ya Mungu illposema, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo akajibu, “Bwana, mimi hapa; nitume
mimi!” (Alikuwa tayari. Alikwisha kuona
kitu fulani. Naam, bwana!)

Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na
aibu;
Sikizeni kilio chao cha huzuni na uchungu;
Hima, ndugu, kimbia ukawaokoe;
Jibu upesi, “Bwana, mimi hapa.”

¹⁹³ Lazima jambo fulani litendwe. Imechelewa kuliko vile tunavyodhania ilivyo. Na ono la Mungu liwashawishi watu, wapate kuona kwamba Mungu yule yule aliyekuwa hekaluni pamoja na Isaya ni Mungu yeye yule katika mahali Pake patakatifu leo. Yeye yuko mahali patakatifu pa Roho Mtakatifu. Yeye ndiye Roho Mtakatifu. Wakati mmoja Yeye alikuwa mwili; sasa Yeye ndiye Roho akitenda kazi kati ya watu Wake, akijionyesha kwamba yu hai, si kanuni za imani zilizokufa, bali Kristo aliye hai, yeye yule jana, leo, na hata milele. Lo, Isaya, jibu upesi, “Bwana, hapa; nitume mimi.”

Na tuombeni. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa . . .

Kaa la moto lilipomgusa nabii,
Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo
kuwa, Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo akajibu, “Mimi hapa; nitume mimi!”
(Pamoja.)

Nena, Bwana wangu; Nena Bwana wangu.
Nena, nami nitakujibu upesi.
Nena, Bwana wangu; Nena, Bwana wangu.
Nena, nami nitajibu, “Bwana nitume mimi!”

¹⁹⁴ Naam, huenda ikawa ni jirani yako; huenda ikawa ni mwanamke unayefanya kazi naye, mwanamume unayefanya kazi naye, bali kuna . . .

Mamilioni sasa wanaokufa katika dhambi na aibu;
(Katika kanuni za imani na madhehebu.)
Lo, sikizeni kilio chao cha huzuni na uchungu.
Hima, ndugu, kimbia ukawaokoe;
Jibu upesi, “Bwana, mimi hapa!”

Nena, Bwana wangu; Nena, Bwana wangu
(Naliona ono kutoka kwa Bwana; nililionia ikitendeka.)
Nena, nami nitajibu upesi (Yeye ameisha nena sasa.)
Nena, Bwana wangu; Nena, Bwana wangu
Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi!”

¹⁹⁵ Basi, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nashangaa usiku wa leo, kama nilivyowaambia nilipokuwa nikija humu, najaribu kusoma kirefu jambo ninalojua lingewasaidia. Mlimwona huyo nabii; alikuwa mtu mkuu. Alizaliwa kusudi awe nabii. Alitambua ya kwamba alikuwa ameshika njia mbaya; alikuwa akimtegemea Uzia, mfalme. Akaona ya kwamba hauwezi kutegemea mikono ya mwili. Huo huangamia. Ni kosa. Bali inua macho yako umwone Mungu ameketi juu sana kwenye kiti Chake cha enzi. Mtazame Yesu pale; Yeye alisema, “Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Hebu na akuinue juu katika Roho. Angalia uone kama si yeye yule jana, leo, na hata milele . . .

¹⁹⁶ Wakati huyo maskini Isaya alipoona ono la Mungu likishuka na kuingia hekaluni, alikuwa tayari kukiri makosa yake. Alikuwa tayari kukiri ya kwamba hakuwa amefanya cho chote chema. Naye basi si aliruka akaenda kule nchini; si alitenda kila kitu kilicho chema wakati huo. Kila kitu ambacho angeweza kufanya, hata hatimaye akatia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake.

¹⁹⁷ Nafikiri huko kungekuwa kujisikia kwetu sisi sote. Wangapi wanajisikia ya kwamba mnetaka kusema—kumsikia Mungu akisema—ya kwamba ungetaka—ungesema kwa Mungu, “Mimi

hapa; nitume mimi!” Inueni mkono yenu. “Mimi hapa, hebu nikamshuhudie muuza maziwa. Hebu nikashuhudie kwa—kwa mtu ye yote niwezaye, nitende jambo fulani. Hebu nitende jambo fulani. Bwana, mimi si—siombi niwe mhubiri. Siombi kuwa hili, lakini, Bwana, kama mimi ni mkulima, nifanye mkulima awezaye kumshuhudia jirani yangu mkulima. Hebu niwe mkulima hata ninapouza nafaka zangu, naweza kumshuhudia mnunuzi wa nafaka. Hebu niwe mkulima.” Kama mimi ni—kama mimi ni mwanamke hebu nimshuhudie mtu wa bima. Hebu nimshuhudie mtu wa maziwa, muuza gazeti. Hebu nifanye jambo fulani, Bwana. Hebu niende karibu na kwetu na nipate kibali kwa dada yangu hapa karibu na kwetu ambaye ni mwovu na amekosea. Hebu nimtolee ushuhuda kwa utamu. Hebu nifunike uso wangu kwa mabawa ya unyenyekevu; hebu nifunike miguu yangu vivyo hivyo. Hebu niwe na kicho Mbele Zako, bali unitume kwa mabawa mawili zaidi, Bwana, kwa mtu fulani, ‘Mimi hapa; nitume, nitume mimi!’”

¹⁹⁸ Kwa hali kama hii hebuni sote tusimama na kujiweka wakfu kwa utumishi wa Mungu. Aliye Mwenyezi yuko hapa. Mnaamini hivyo? Tuko katika Uwepo Wake wa Kiungu. Msisahau hilo sasa. Uwepo Wake umo papa hapa kama tu ulivyokuwa. . . Bila shaka, tangu niliposimama hapa, nimeona maono manne matano yakitokea. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wamekuwa na zaidi ya watu wawili watatu walio wa kanisa hili ambao hawakusema kitu; bali Uko hapa vivyo hivyo tu. Sawa.

Sasa, tunachotaka kufanya, kila mmoja wenu kwa njia yunu wenyewe, hebu na tujiweke wakfu kwa Mungu.

Tunaona ishara zikionekana za kuja Kwake kwenye heri;

Lo, tazama, mtini unatoa majani.

Injili ya Ufalme imeenezwa katika kila taifa, Nasi tumekaribia; mwisho unaweza kuonekana.

(Hiyo ni kweli. Hiyo si kweli?)

Basi kwa furaha; tutatangaza mbele Ujumbe wa kuonekana Kwake kwenye heri;

Hivi karibuni Yeye yuaja katika utukufu kumwambia mmoja ma wote.

Basi amkeni enyi watakatifu wa Bwana.

Mbona mnasinzia huku mwisho unakaribia, Hebu tujitayarisha kwa ajili ya huo mwito wa mwisho

(Amina!)

Mataifa yanavunjika; Israeli inaamka (ni taifa sasa.)

Ishara walizotabiri manabii, Siku za Mataifa zimehesabiwa

Huku zimelemewa na hofu, (Mnaona ikija kule
ng'ambo, si mataifa tu, bali makanisa.)
Rudini makwenu, Enyi mlio chukiwa.

Siku ya ukombozi imekaribia;
Mioyo ya watu ikivunjika kwa hofu.
Jazweni na Roho,
Taa zenu zitengenezwe ziwe safi;
Inueni macho yenu, ukombozi wenu
umekaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya;
Ukweli wa Mungu wanaukana;
Ya kwamba Yesu, aliye Kristo, ndiye Mungu.
(Mnajua wanafanya hivyo.)

Bali—bali tutatembea walikokanyanga
mitume.

Kwa maana siku ya ukombozi imekaribia;
Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu;
Jazweni na Roho,
Taa zenu zitengenezwe ziwe safi,
Inueni macho yenu, ukombozi wenu
umekaribia.

¹⁹⁹ Futilia mbali huo moshi wa kidhehebu. Futilia mbali haya masizi ya kilimwengu. Damu ya Yesu Kristo yatosha zaidi kukusafisha wewe. Inueni macho yenu! Hebu muru zenu ziwe zinaangaza. Chukueni hayo mabawa mruke kwa mtu fulani moja kwa moja.

Hebu tuinue mikono yetu sasa tusema, “Mungu, mimi hapa; nitume mimi.”

²⁰⁰ Baba uliye Mbinguni, najiweka wakfu Kwako usiku wa leo, Bwana, pamoja na kanisa hili, baada ya ujumbe huu, mkali, mgumu, “Mimi hapa, Bwana, nitume mimi.” Kanisa langu liko hapa Bwana. Na wao wafunike nyuso zao katika kicho. Na wafunike miguu yao katika unyenyekevu. Na wapate ujasiri kuruka na Ujumbe, upesi, kwa mtu mwingine. Tujalie, Bwana. Na washuhudie kwa utamu, wawe chumvi ya dunia iliyo na Mwokozi ndani yake. Bwana Mungu, hii ndiyo sadaka yetu. Hili ndilo toleo letu. Hizi ndizo shukrani zetu. Hii ndiyo tunayotaka sana, Bwana. Tutume usiku huu kwa mtu aliyepotea. Na tuwavute tuwapeleke kanisani kesho mahali fulani. Na tuwafundishe njia ya Bwana. Hebu wao waokolewe, Bwana, kwa maana kumechelewa kuliko tunavyodhania. Tujalie, Bwana.

²⁰¹ Na tukusudie hili mioyoni mwetu. Tunapolinena, Bwana, chukua kaa la moto wa Roho Mtakatifu kutoka madhabahuni Kalvari; gusa kila moyo na mdomo usiku wa leo, Bwana, tuiseme uongo wo wote, tupate kunena yaliyo Kweli. Tuchukue usiku wa leo, Bwana, jinsi tu tulivyo. Sote si wahubiri. Sote si manabii. Sote hatuneni kwa lugha. Sote hatufanyi miujiza;

bali sisi sote tuna jambo la kufanya. Tuonyeshe lilipo, Bwana. Tushuhudie, tuimbe, ama tuombe. Na kama mikate iliyo juu ya maji, itarudi siku moja yenye utukufu. Tujalie, Bwana. Tuko hapa. Tutume kwa jirani zetu po pote tuwezapo, kwa wenzetu, tukawaambie habari za kuja kwa Bwana. Tujalie, Baba.

²⁰² Tubariki sasa. Hebu na tupate mapumziko mazuri miilini mwetu usiku wa leo. Hebu na tuamke tuje kanisani asubuhi; ukaweze kunena kwa—kwa nguvu sana kesho, kwamba Wewe hutaacha jiwe hata moja lisilopinduliwa, ili kila mtu apate kujua jinsi ya kuingia kitika hili. Tufundishe, Bwana. Tunangoja. Tufundishe mnamo asubuhi jinsi ya kufikia kimo hiki kikamilifu ambapo tunaweza kuwa wana na binti za Mungu. Tunakungoja Wewe, Bwana, huku kaa la moto likiwa tayari kuwekwa midomoni mwetu. Tunangoja, Baba, katika Jina la Yesu.

²⁰³ Basi huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Nitamuuliza mchungaji basi aje huku mbele apate kufunga ibada. Mungu awabariki. Natumaini kuwaona asubuhi sasa. Mungu awe pamoja nanyi, awaponye wagonjwa wote na wanaoteseka miongoni mwetu, amfanye kila mmoja wenu...Najisikia nimejazwa na Roho hivi sasa. Namsikia Roho Mtakatifu. Nasikia Uwepo Wake. Najua Yeye yuko hapa. Nina hakika Yuko hapa. Ninamwona Yeye; ninajua Yeye yuko hapa. Namwona akienda, hiyo Nguzo kuu ya Moto. Utukufu! Naona lile dhahirisho la Utu Wake, uungu wa Uwepo Wake...?...Utukufu mkuu wa Utu Wake. Mungu, rukaruka juu ya watu hawa; hebu na ye yote kati yao asipotee, naomba. Utukufu kwa Mungu!



USHAWISHI WA MWINGINE SWA62-1013
(The Influence Of Another)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, October 13, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org